TAZAMA ALIKO YESU

Amina. Ahsante, George, Becky, na Dada Ungren, wimbo mzuri huo! Hiyo ni kweli, "Yote yanabadilika Yesu anapokuja." Yeye hufungia tu giza nje, na kusambaza ile Nuru, nasi tunashukuru kwa ajili hiyo. Sasa, hiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Becky kupiga kinanda kanisani hapa, kwa hiyo wimbo unaostahili sana, *Yesu Alipokuja*.

2 Kwa hiyo tunashukuru kuwapo hapa tena, usiku wa leo, na tunashukuru sana kwa ajili ya...uhudhuriaji wenu mzuri asubuhi ya leo. Na sasa usiku huu, ni, ninalo somo dogo ninalotaka kuzungumza juu yake, katika muda mfupi; lakini kabla tu ya hilo, ninayo baadhi ya matangazo nitakayofanya, na kadhalika.

3 Nami kidogo tu nimepwewa. Nafikiri ni kule tu kuzungumza kupita kiasi. Nilihubiri muda mrefu. Lakini ninapochukua hizi, kanda, za saa moja au mbili, nami ninaporudi hapa, ni kwa sababu ninazinasa hizo kwa ajili ya ulimwengu mzima. Na kwa hiyo ninawashukuru kwa kuwa wavumilivu sana kwetu asubuhi ya leo.

4 Na sasa kuna mambo machache ambayo ningetaka kuyataja hapa. Na hayo ni, kwamba, ni—ningengetaka kuliuliza kanisa, jambo la kwanza, kitu ambacho nime—nimekifanya, nami na—nataka kuuliza kama naweza kukibadilisha hicho, usiku huu. Sisi hatu-...

5 Mimi siweki nadhiri za mwaka mpya. Ndipo nita... inatupasa kwenda nyumbani kesho, kwa hiyo sisi hatutakuwa hapa kwa ajili ya mwaka mpya, ku-...lakini tutakuwa tunawakumbuka. Nami naamini kutakuwa na mkutano hapa, usiku wa mwaka mpya. Naam, hiyo ni kweli, i—ibada ya kukesha, kama sikuzote walivyo nayo usiku wa mwaka mpya. Tungependa kubaki, lakini basi hatuwezi kuwahi kurudi ku—kuwapeleka watoto shuleni. Na mke wangu yampasa kufua nguo zao; mnajua jinsi ilivyo.

6 Kwa hiyo nataka kumshukuru kila mmoja wenu kwa ajili ya mambo yenu mema mliyotutendea katika Krismasi. Nanyi wanawake mliokwenda juu kule na kuweka chakula nyumbani, na kadhalika, kwa ajili yetu, ili kwamba tulipofika kule—kule, vitu hivyo vilikuwa vimeishapikwa na tayari kwa kuliwa. Bila shaka nawashukuru kwa ajili hiyo. Mungu awabariki daima.

7 Nalo kanisa, kwa ajili ya stakabadhi yao ndogo, kwamba ningeliweza kwenda hapa na ku—kupata baadhi ya nguo kama ningezitaka, kwa ajili ya suti. Wao hunipa mimi suti kila mwaka. Na baadhi ya rafiki zangu wema walinipa tu suti. Kwa hiyo nafikiri, kama ni sawa, mimi nahitaji baadhi ya vitu vingine

kama mashati na fulana, na kadhalika, ningependa kuchukua zile fedha katika hivyo kama ni sawa kwa kanisa. Mimi nahitaji hivyo zaidi ya ninavyo . . . kuzidi ninavyohitaji suti, wakati huu.

8 Na sasa, huyu jamaa mdogo ambaye ndiyo kwanza atuimbie, Ndugu George Smith, kutoka kule Tucson, tumekuwa tukienda kwenye kanisa lao juu kule, lile kanisa la Batisti la Agano Jipya. Baba yake ni mmishenari. Nafikiri anayo yapata makanisa saba huko Old Mexico. Na bila shaka kuna baadhi ya watu wazuri kule. Na baba yake na mama, nao hao wote, ni watu wazuri. Naye George ni kijana mzuri sana. Nilisikitika tu kwamba hakutupa ushuhuda mfupi kabla hajaketi chini, wa neema ya Kristo inayookoa katika maisha yake.

9 Basi, zile—zile Jumbe, niliahidi hapa si muda mrefu uliopita, ya kwamba zile Jumbe, kabla sijaenda kule nje katika mikutano, ningekuja hapa na kuzinasa kwanza na kisha niende kule nje. Hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya kupeleka kanda kwa watu. Kisha ningekuja hapa na kunasa Ujumbe, kisha niende nje na kuuhubiri Huo. Hilo lingewapa watu nafasi, kwa wa—wanaonasa kanda, kuzinasa zile kanda na tuzichukue tunapokwenda. Sasa najiandaa kuondoka kwa ziara ndefu ya uinjilisti, kwa hiyo sita—sitaweza kufanya hivyo kuanzia sasa na kuendelea, mnaona, na yule anayenasa kanda itampasa kuzinasa tunaposafiri.

10 Nami nafikiri, hata hivyo, si watakuwa na mkutano wa kanda juma hili? Au, jambo fulani ama jingine kuhusu, jambo fulani kuhusu kanda juma hili. Kwa vyo vyote, nafikiri Ndugu Sothmann yuko hapa, naye anamwakilisha Ndugu Maguire. Sijui kama yeye yuko hapa au la. Nafikiri Ndugu Fred yuko hapa. Mtu fulani alisema alikuwa hapa. Naye . . . Nafikiri wao wana mkutano juma hili, labda kesho usiku, au wakati fulani, kuhusu kanda. Tulikuwa tukizungumza kuhusu hizo jujuzi usiku, kule chumbani. Nafikiri wakati umewadia kwa ajili ya jambo fulani, kwamba wachukue na kufanya mipango kuhusu hilo.

11 Kwa hiyo, tangu sasa na kuendelea, huenda nitazungumza tu Jumbe ambazo sijazigusa hapa kwenye Maskani, huko nje mikutanoni.

12 Na sasa ninayo, nataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya ushuhuda huo wa Ndugu Blair. Imetukia kwamba Ndugu na Dada Blair wameketi papa hapa usiku huu, wanaketi papa hapa mbele zetu, yule ambaye alikuwa na yule mvulana mdogo. Nami nakumbuka wakati Bwana aliponiambia, wakati yeye alipokuwa . . . Ndugu Blair, amefadhaika kabisa, analia. Na mvulana wake mdogo alikuwa amepondapondwa usoni namna *hii*, na gari lililopinduka, naye alikuwa mahututi sana. Lakini nilipokuwa ni—nikiomba, nilimwona yule jamaa mdogo akiwa

mzima. Ndipo Ndugu Blair, bila shaka, akaniuliza, akasema, "Ndugu Branham, hili ni BWANA ASEMA HIVI?"

Nikasema, "Ndugu Blair, Blair, ni BWANA ASEMA HIVI."

13 Na Ndugu Blair yuko hapa usiku wa leo. Nasi bila shaka tunashukuru kuwa na Ndugu Blair pamoja nasi. Naye amekuwa akiugua u—ugonjwa mdogo wa kushikwa na wasiwasi. Basi Shetani alimpa pigo kubwa, hapa si muda mrefu uliopita, akijaribu kumfanya kutokuniamini mimi. Na wakati Shetani alipokuwa akifanya hivyo, Bwana alikuja karibu na kumfunulia jambo hilo; na kumwambia habari zake, kulikatiza tu kabla wakati haujafika kwa ajili ya hili. Naye Ndugu Blair ni mtu mzuri. Nami nawataka mumkumbuke. Yeye amesimama katikati ya maoni kwamba afanye nini. Hajui tu ageukie upande gani. Nami nasadiki, Ndugu Blair, kwamba Mungu . . . Wewe u mtumishi mashuhuri wa Kristo, Naye anayo mambo tele kwa ajili yako kutenda, sababu Nuru zinafifia. Ulikuwa hapa asubuhi ya leo? Aha-aha. Vema, hilo ni zuri sana.

14 Basi—basi, nadhani, mara ya pili nitakapowaona, huenda itakuwa katika msimu wa Kuchipua, kidogo tu. Basi ifikiapo wakati huo, huenda tutajua kama tutafanya ile mi—mikutano, au la, hapa Jeffersonville, mnamo wakati ambao ningelikuwa Norway na katika nchi za Scandinavia. Sasa kabla tu hatujachukua somo . . .

15 Sababu, tunao mstari wa maombi unaokuja, na wengi wamesimama, vyumbani, na kandokando ya kuta, na kadhalika, nami najua, ninyi, ni hali ngumu kwenu. Nami nilisimama, mara nyingi, mimi mwenyewe. Nami nilipita, muda kitambo uliopita, nikimleta mke wangu, nikawaona watu milangoni. Basi nikawaza, "Nani anasema Injili bado siyo kitu kinachovutia zaidi kilichoko ulimwenguni?" Hakika ndiyo. Ndiyo, Hiyo inawavutia hao ambao wanaipendelea Hiyo. Nao ambao hawaipendelei, bila shaka, hawavutiwi. Wao, Hiyo haitawavutia. Bali, Yesu, "Kama," kasema, "kama mimi nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu Mimi." Hilo ni kweli jinsi gani!

16 Na wakati ninapofika hapa, kuna mengi sana ya kusema, nami kwa namna fulani sina budi kuandika mambo nitayozungumza hapa, kwa kitambo. Au mimi . . . Kuna mengi sana ya kusema, hata unasahau mambo utakayozungumza.

17 Sasa, nasikia kwamba baba yake Ndugu Ungren alibatizwa asubuhi ya leo, katika Jina la Yesu Kristo. Na kama Dada Ungren na wengineo wako hapa, nina hakika hilo ni jambo kuu kwao, kwa sababu hayo yamekuwa ni maombi yao ya sikuzote kwa miaka mingi. Basi Ndugu Ungren, popote ulipo, Mungu akubariki sana, ndugu yangu.

18 Na kama hilo si sahihi, Mungu atanipasisha hilo kwenye Siku ya Hukumu. Mnaona? Najua ni sahihi. Ni—nitachukua lawama ya hilo. Hilo ni sawa kabisa, kwa sababu ni Kweli.

Wasema, "Je linaleta tofauti yo yote?"

19 Lilifanya hivyo kwa Paulo. Waliuliza jinsi walivyobatizwa. Walisema walikuwa tayari wamebatizwa na Yohana, mtu yule aliyembatiza Yesu. Paulo alisema iliwapasa waje wakabatizwe tena, katika Jina la "Yesu Kristo." Na hakuna mtu hata mmoja katika Biblia aliyewahi kubatizwa katika Jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

20 Hakuna watu waliowahi kubatizwa namna hiyo hadi kule kuundwa kwa kanisa Katoliki katika Lao . . . Lao-Nikea, Baraza la Lao-Nikea pale Lao-Nikea, Rumi. Hapo ndipo yule mtu wa kwanza aliwahi kubatizwa, kwa kutumia vyeo.

21 Mtu mmoja alisema nami majuzi. Nilisema, "Vema, kama . . . Yule 'Bwana Yesu,' hilo ni Jina Lake." Akasema . . . "Vema," nikasema, "kama mtu akija kwako . . . "

Alisema, "Sidhani linaleta tofauti yo yote."

22 Nilimnasa tu katika fundisho lake mwenyewe. Nikasema, "Kama mtu akija kwako na kusema, 'Nimebatizwa katika Jina la Waridi la Uwandani, Yungiyungi la Mabondeni, na Nyota ya Asubuhi,' ungesema 'amina' kwa hilo?"

Akasema, "Hapana, bwana."

Nikasema, "Jinsi gani . . . Ungembatiza tena?

Kasema, "Ndiyo, bwana."

Nikasema, "Ungembatiza jinsi gani?"

Akasema, "Ningembatiza huyo katika Jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

23 Nami nikasema, "Hiyo ndiyo njia ningembatiza huyo, ndiyo, katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Nikasema "Basi, 'Waridi la Uwandani, Yungiyungi la Mabondeni, na Nyota ya Asubuhi' si jina."

Akasema, "Hiyo ni kweli. Ni cheo."

24 Nikasema, "Vivyo hivyo 'Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.' Basi ningembatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; na Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni 'Bwana Yesu Kristo.' Kabisa. Kwa hiyo nasema . . . " Naye akaliona.

25 Huyo alikuwa Ndugu Joseph Mattsson-Boze, wa Chicago, mtu ngumu sana niliyewahi kufaulu kumpata, kwa huo. Nami nadhani ninao yapata wenyeji elfu tatu au elfu nne wa kubatizwa sasa, wakati nitakapofika kule Afrika pamoja naye, na kuwabatiza tena.

26 Basi, kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya Nuru ya Injili. Na kwa hiyo basi, Yesu alisema, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, "Mimi, ninayoyasikia, ndiyo ninenayo." Na sasa nitasema . . . Kwa ninino zetu zifuatazo tu, yapata dakika kumi, au kumi na tano, kabla tu sijachukua somo langu, na ni somo fupi sana, na kisha tutakuwa na mstari wa maombi. Nimefikia mahali katika huduma yangu, ambapo mimi ni . . . yanipasa ku—kusema jambo fulani. Nami . . .

27 Yesu alisema hilo. Kwamba lile Yeye alilolisikia, hilo ndilo Yeye alilonena. Kisha akasema, "Niliwaita rafiki Zangu, naye rafiki huwaambia rafiki zake mambo yote."

28 Paulo alisema, katika Matendo 20:27, "Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya Kusudi lote la Mungu." Mnaona?

29 Nami hebu nijiunge, usiku wa leo, na kusema jambo lile lile pamoja na huyo mtakatifu mashuhuri wa kale. Kwa kadiri nijuavyo, sijajiepusha . . . sijajiepusha, ila nimewahubiria Kusudi lote la Mungu.

30 Mtu mmoja alikuwa akicheza mojawapo ya kanda, majuzi. Na kwa sababu tu ilimfanya mtu fulani akasirike, waliwatupia risasi kupitia dirishani, na mwanamke mmoja akajeruhiwa.

31 Kwa hiyo huenda siku moja nitatia muhuri ushuhuda wangu. Lakini wakati huo ujapo nao . . . niko tayari kwenda. Hadi wakati wangu ujapo, hakuna kitu kitakachoniumiza mimi hadi wakati huo. Mnaona?

32 Basi, tunaamini katika Injili ile ile, jinsi hasa Biblia imeandikwa. Imelengwa. Na—na kama bunduki imelengwa, na iko tayari; kama ikipiga lengo mara ya kwanza, itapiga hilo mara ya pili, na kila mara.

33 Kama mti, au tawi, mzabibu, ukitoa tawi, na tawi hilo lizae tunda fulani; mara ya pili ule—ule mzabibu ukitoa tawi, litazaa aina ile ile ya tunda.

34 Na kama Yesu ni Mzabibu, na sisi ni matawi; na Tawi la kwanza, Kanisa, ambalo huo Mzabibu ulitoa, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Na hilo Tawi la kwanza walibatiza katika Jina la Yesu Kristo. Nao walikuwa na Mungu aishiye miongoni mwao, ambaye alifanya mambo yale yale miongoni mwao ambayo Yeye alifanya wakati alipokuwa duniani. Kwa hiyo, watu wakawatambua, ijapokuwa walikuwa wasio na elimu na wasio na maarifa, ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu, kwa sababu Uhai Wake ulikuwa ndani yao.

35 Kama nilivyosema, kama nilikuwa na roho ya—ya Beethoven ndani yangu, ningeandika nyimbo. Kama Beet . . . kama mimi . . . Kama Bethoven aliishi ndani yangu, ningekuwa Beethoven. Mnaona?

36 Kama Shakespeare aliishi ndani yangu, ningekuwa Shakespeare. Ni—ningeandika mashairi, na—na—na michezo ya kuigiza, na kadhalika, kama Shakespeare aliishi ndani yangu.

37 Na kama Kristo anaishi ndani yangu, kazi za Kristo utazitenda. Sawa. Hapana budi iwe namna hiyo. Na Kristo ni nini? Neno. Yeye alisema, "Kama mkikaa ndani Yangu. Neno Langu ndani yenu, basi ombeni lo lote mtakalo; litatendwa." Kwa sababu, Neno liko pale, linahitaji tu Nuru; na Nuru hulifanya Hilo liishi.

38 Kwa hiyo sasa nitawaambia jambo fulani, sasa, ambalo sijasema hadi sasa. Na, hilo ni, jambo ambalo tumelitazamia kwa muda mrefu sana (kwa kadiri ya miaka mingi, miaka minne au mitano, au labda muda mrefu zaidi), ule Mvuto wa Tatu, sasa umethibitishwa, nami nina hakika nyinyi nyote mnajua huo ni nini.

39 Sasa kumbukeni, kamwe hakutakuwapo na kuigizwa kwa huo, sababu hauwezi kuigwa. Mnaona, hauwezi kuigwa. Sasa upo. Nami nina . . . nimeonywa juu ya jambo hili, ya kwamba hivi karibuni . . . Umetukia wakati uu huu hasa, ili kwamba uweze kutambulisha uwepo wake miongoni mwenu, mnaona, bali hautatumika sana mpaka Baraza hili lianze kukaza. Na litakapofanya hivyo, jambo hilo litakapotukia . . . Wapentekoste, na kadhalika, wanaweza karibu kuigiza cho chote kinachoweza kutendwa. Bali wakati huo ujapo, wakati kule kufinywa kutakaposhuka, ndipo mtaona, yale mmeona kwa kitambo, yakidhihirishwa katika ule utimilifu wa nguvu zake. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Mnaona?

40 Sasa lazima niendelee katika uinjilisti. Kama tu vile nilivyoagizwa, kwanza, lazima niendelee. Kwa hiyo, mmekuwa na Neno, na mnajua mnachopaswa kutazamia, na jinsi ya kusimama. Ni lazima niendelee katika uinjilisti. Na, rafiki zangu, tulieni, na mwendelee tu kusonga mbele, kwa maana ile saa inakuja mbio, mnaona, ambapo wakati jambo fulani litatendwa.

41 Sasa, mwaweza kuona baadhi ya vitu vidogo visivyo vya kawaida vikitukia kwangu. Si dhambi; simaanishi hilo. Bali, namaanisha, kitu cha kipekee mbali na mwelekeo wa kawaida. Kwa sababu, mahali nilipofika sasa, katika huduma, ninarudi nyuma hapa, nikichungulia mahali pale na kungojea wakati wa kuutumia. Bali, utatumika.

42 Na kila mmoja anajua ya kwamba, basi, kadiri ule wa Kwanza ulivyotambulishwa dhahiri, vivyo wa Pili umetambulishwa. Na kama mtafikiri kwa makini, nyinyi ambao ni wa kiroho. Kama Biblia ilivyosema, "Hapa ni kwake yeye aliye na hekima." Ule wa Tatu umetambulishwa vizuri. Mnaona? Tunajua mahali ulipo. Kwa hiyo, ule Mvuto wa Tatu uko hapa.

43 Ni mtakatifu sana, hivi kwamba, sipaswi kusema mengi kuuhusu huo. Kama Yeye alivyoniambia pale mwanzo, kasema, "Huu, usiseme lo lote kuuhusu." Mnakumbuka hilo, miaka mingi iliyopita? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Huo unajielezea wenyewe. Mnaona? Bali, pia, nimejaribu kueleza ile mingine, nami nilikosea. Huu utakuwa ndicho kile kitu, ambacho, kwa maoni yangu. . .Sisemi Bwana ananiambia jambo hili. Huu utakuwa ndio kile kitu ambacho kitaanzisha ile imani ya Kunyakuliwa, kwa ajili ya kuondoka. Mnaona? Mnaona? Nao. . .

44 Ni lazima nikae kimya kwa muda kidogo tu. Sasa kumbukeni, nanyi ambao mnasikiliza kanda hii, mnaweza kuona badiliko kama hilo katika huduma yangu sasa hivi, kushuka chini, siyo kwenda juu; kushuka chini. Tuko hasa kwenye ule wakati sasa, na haiwezi kuwa, haiwezi kusonga mbele zaidi. Yatupasa kungojea pale kwa dakika moja tu mpaka jambo hili litukie *hapa*, kuwahi, kisha ule wakati utafika. Bali, huo umetambulishwa kikamilifu.

45 Unakuja wakati ambapo, katika taifa hili, mahali ambapo hili taifa litatumia uwezo wote ambao yule mnyama aliyelitangulia alikuwa nao, ambaye alikuwa ni Rumi ya kipagani wakati ilipofanyika Rumi ya upapa, mnaona, ambapo hili taifa litafanya hivyo.

46 Ufunuo 13 inaeleza hilo waziwazi. "Yule mwana-kondoo alipanda juu kutoka katika nchi. Yule mnyama mwingine alipanda juu kutoka katika maji," wingi na makutano ya watu. Huyu mwana-kondoo alipanda juu mahali ambapo hapakuwa na watu. Mwana-kondoo huwakilisha dini. Mwana-kondoo wa Mungu. . .Na, kumbuka, alinena kama mwana-kondoo. Alikuwa mwana-kondoo.

47 Ndipo basi, baada ya muda, akawa. . .akapokea uwezo, kisha akanena kama joka; na kutumia ninino wote—yule joka, uwezo wa yule joka mbele yake. Na yule *joka* ni "Rumi," sikuzote. Kwa hiyo basi hamwoni? Madhehebu ya Kirumi; "alama," madhehebu ya Kiprotestanti; "sanamu ya mnyama," yakiunda mamlaka itayolazimisha Waprotestanti wote, kama muungano. Itakupasa kuwemo katika Baraza hili la Makanisa, la sivyo hutaweza kufanya ushirika. Au ku--ku-. . .

48 Naam, kwa kweli ndivyo—ndivyo inavyotendeka sasa. Huwezi kwenda kanisani na kuhubiri isipokuwa unayo kadi ya ushirika au aina ya kitambulisho. Na sasa, kwa watu kama sisi, tutatengwa na hayo yote, kabisa, hiyo ni sahihi, sababu hawataweza kufanya hilo.

49 Inakazwa zaidi. Na kisha wakati huo ujapo, na kule kufinywa kunafikia mahali ambapo mnafinywa hata mkatolewa nje, ndipo tazamieni ninayojiandaa kuwaelezeni katika dakika chache. Utazamieni ule Mvuto wa Tatu wakati huo, mnaona, nao

bila shaka utakuwa ni kwa ajili ya waliopotea kabisa, lakini u-- utakuwa kwa ajili ya Bibi-Arusi na Kanisa.

50 Sasa tuko karibu zaidi kuliko inavyoonekana kuwa. Sijui ni lini, bali ni karibu sana, sana. Huenda ikawa najenga jukwaa kusudi mtu mwingine apate kuipanda. Huenda nikachukuliwa kabla ya wakati huo. Sijui. Na wakati huo waweza ukawa ni juma hili lijalo, ambapo Roho Mtakatifu atakuja pamoja . . . na kumleta Kristo Yesu. Yeye anaweza kuja juma hili lijalo. Yeye bado anaweza kuja usiku huu. Sijui Yeye atakuja lini. Yeye hatwambii hilo.

51 Bali naamini, kwamba tuko karibu sana, hata nisingeweza kamwe kufa kwa uzee. Hata hivyo, kwa umri wa miaka hamsini na minne, siwezi kamwe kufa kwa uzee, hadi Yeye yuko hapa. Mnaona? Isipokuwa nipigwe risasi, niuawe, ama cho chote kile, kwa njia fulani nivawe, uzee tu hauwezi kuniva, mpaka Yeye amekuja. Nami naamini hilo.

52 Nami nataka kusema hili. Sijawahi kulisema awali. Bali kulingana na Maandiko, kulingana na aliyosema Yeye miaka thelathini iliyopita; miaka thelethini na mitatu iliyopita mtoni kule chini, mwaka 1933, hasa; aliyosema Yeye, kila kitu kimetukia sawasawa kabisa. Huenda nisitende hilo, bali Ujumbe huu utamjulisha Yesu Kristo kwa walimwengu. Kwa maana, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kwa kwanza, vivyo hivyo huu Ujumbe utakutangulia kule Kuja kwa pili." Naye Yohana alisema, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Mnaona? Kwa hiyo, una-, unaenda sambamba nao kwa kila njia. Nami najua utaendelea, huu Ujumbe utaendelea.

53 Basi, kumekuwa na baadhi ya mambo makuu yaliyotukia njiani. Asubuhi ya leo nilikuwa na mahojiano chumbani hapa. Na ki—kijana mmoja, jina lake Autry, yeye huenda bado angali hapa usiku wa leo. Anatoka San Antonio, Texas. Amekuja kuuliza kama . . . wakati tulipokuwa tunakwenda Dallas, kutoka California; kama tungaliweza kutelemka usiku mmoja kwenye maskani yao, kwa usiku mmoja tu. Nao wanatazamia hilo, katika siku moja mbili zijazo, kuona kama tunaweza kufanya hivyo. Naye alikuwa akinieleza kuhusu . . . Sijawahi kufika San Antonio tangu mkutano ule wa kwanza.

54 Basi, ule mkutano wa kwanza, nilipofika San Antonio. Nilikuwa kule, nafikiri, pamoja na Ndugu Coot na—na Shule ya Biblia ya Kimataifa. Nami nasahau ule ukumbi tulimofanyia ibada. Nao ulikuwa aidha usiku wangu wa kwanza au usiku wa pili, nafikiri usiku wa kwanza, nilipokuwa nikienda jukwaani, mtu mmoja alisimama jengoni, kule nyuma kabisa, akanena kwa lugha, kama bo—bombom ikifyatua risasi. Naye hata kabla hajaketi chini, nukta moja ama mbili, kabla mtu mmoja hajainuka pale jukwaani na kutoa tafsiri.

55 Nami nikasimama, kwa hayo aliyosema. Kisha nikamwambia yule mtu, "Je unamfahamu mtu *huyu*?"

Akasema, "La, bwana." Naye akasema . . .

Nikasema, "Ulikujaje hapa?"

56 Akasema, "Wale watu ninaowafanyia kazi, walikuwa . . . walikuwa hapa usiku wa leo, nao wamenileta." Yeye ni . . . alikuwa ni cowboy.

Nami nikasema, "Unafanya kazi gani *wewe*?"

57 Akasema, "Je! wewe unamjua?" Akasema, "La, bwana. Sijawahi kumwona."

58 Nami nikasema, "Wewe unafanya kazi gani?" Naye alikuwa ni—ni mfanya-biashara humo mjini.

59 Na yale waliyonena katika—katika . . . Basi, nilikuwa sikuzote, kabla sijajifunza vyema, nilikuwa kidogo nashuku kunena kwa lugha; nilifikiri nyingi za hizo zilikuwa za kimwili, na huenda zikawa. Bali wakati hii iliponenwa, hiyo tafsiri ilikuwa sawa kabisa na alivyosema yule Malaika wa Bwana kule chini mtoni, miaka kumi na mmoja kabla ya hapo, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, wewe umetumwa kutangulia kwa pili." Mnaona?

60 Nayo ilikuwa hapo, wakati huyo Malaika, hiyo Nuru ambayo imetambulika kikamilifu. Na kanisa,na kwa Neno, kwa sayansi, na kila kitu, kimeitambua. Hiyo Nuru, kwa mara Yake ya kwanza kuonekana hadharani, ikisimama pale hasa nilipokuwa; yapata saa nane alasiri, mwanzo wa lile daraja pale pale, papa hapa chini kwenye mwanzo wa Barabara ya Spring, majini. Sasa, hiyo imekuwa ni miaka mingi, mingi sana iliyopita. Na yale hasa Hiyo ilinena, yamekuja kutimia, kabisa.

61 Huyu ndugu hapa alikuwa akiniambia, asubuhi hii. Alioa msichana kutoka kanisani hapa, binti ya Dada Noyes. Nami sijui, nakisia huyo kijana . . . Je uko hapa, Ndugu Autry? Sijui. Alitoka San Antonio. Sijui kama yuko hapa au la. Alikuwa hapa asubuhi hii. Naye alikuwa akinieleza. Naamini ilikuwa ni babu yake, wakati wa huo mkutano, alikuwa na kifafa maishani mwake mwote, naye aliletwa pale.

62 Huo ulikuwa Mwanzo, mwanzo wa hii huduma, wakati Hiyo ilisema hayo, na ule upambanuzi ulikuwa kuweka mikono yao juu ya mkono wangu, na yale yangesemwa yangekuwa ni vile ilivyokuwa. Nami niliwaambia, na wengi ni mashahidi usiku huu, kwamba ingetukia kwamba ningejua siri hasa za mioyo yao. Mnakumbuka hilo, kabla halijatukia? Yapata miaka mitano au sita baadaye, hilo likatendeka; kule Canada, kwa mara yake ya kwanza, na hilo likatukia. Kisha Yeye akasema, "Kama utaendelea kuwa mwaminifu, itakuwa tu ikiendelea." Na sasa lile jambo la Tatu limetukia, mnaona, ikienda tu sikuzote mbele.

63 Naye alisema baba yake aliletwa mstarini, na kuambiwa juu ya hiki kifafa, na kadhalika, na maombi yakafanywa kwa ajili yake. Na hiyo imekuwa ni miaka kumi na sita iliyopita, nafikiri ndivyo ilivyo, yapata miaka kumi na sita au kumi na saba iliyopita. Naye anasema hajawahi kushikwa na hicho tangu wakati huo. Naye karibu ana karibu umri wa miaka themanini na mitano, naye kamwe hakijamshika tangu wakati huo. Ni nini? "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

64 Je Margie Morgan yuko jengoni? Dada Margie Morgan, bibi aliyekuwa ameliwa na kansa; nesi. Ni wangapi wanamkumbuka Dada Morgan? Kama yuko hapa, hawezi kuingia ndani. Alikuwa anauguza. Mnaona, alikuwa kwenye orodha ya wenye kansa huko Louisville, huyo mwanamke amekufa kwa yapata miaka kumi na sita, kumi na saba, kwenye orodha ya wenye kansa huko Louisville.

65 Wakati Jim Tom Robertson, yule mwanasheria, mwanasheria Mkristo, aliposikia kuhusu hilo, alikwenda kwenye Hospitali ya Wabatisti, kuchunguza aone kama ilikuwa ni kweli, kwa maana baba yake yuko kwenye halmashauri, ni mdhamini katika Hospitali ya Wabatisti. Nao walikichunguza kisa hicho, na yule mwanamke alidhaniwa alikuwa amekufa, miaka mingi iliyopita. Naye anauguza hapa Jeffersonville, hospitalini. Aliposimama papa hapa, wakati ilipowabidi kushikilia, hata akili zake zilikuwa hazifanyi kazi. Bali ilikuwa BWANA ASEMA HIVI, naye anaishi. Alikwenda kuuguza, huko Louisville.

66 Na jamaa mmoja hapa, kwenye Duka la Peremende la Schimpff. Je! Bw. Schimpff yuko hapa usiku wa leo? Ningetaka yeye ayasimulie, kama yuko hapa. Sonny Schimpff, mtu mkubwa mwenye afya. Mara nyingi nilipozoea ku . . .

67 Nachukia kusema hili, bali ni ukweli. Baba alizoea kunipa senti kumi kama nilifanya kazi juma nzima, nami ningekuja mjini na kuegesha baiskeli yangu karibu na nyumbani mwa Ndugu Mike Egan, mmoja wa wadhamini hapa. Pamoja na Jimmy Poole, nafikiri mwanawe yuko hapa usiku wa leo; Jim na mimi, na Earnest Fisher, nasi tungeshuka tukaenda mjini, kisha tukaenda kuona sinema kwa senti tano, nasi tulikuwa tukiona zile sinema za kale zilizotulia. Tulikuwa watoto wadogo, na tulitaka kufanya hivyo, yapata umri wa miaka minane, kumi. Tulikuwa na huyo William S. Hart. Wengi wenu ninyi jamaa hamumkumbuki, yule mcheza sinema wa kale. Sinema zilizotulia; nami nisingaliweza kusoma. Ilinibidi kutazama tu yaliyokuwa yakitendeka. Nayo ingepaswa kufafanua hayo yote, nami nisingaliweza kuelewa hayo, bali ningetazama aliyokuwa akitenda.

68 Nami ningekuwa na senti tano zilizosalia. Basi ni wangapi wanakumbuka wakinunua barafu za koni kwa senti moja? Sawa. Ningaliweza kupata barafu tatu za koni, na peremende kali za

thamani ya senti mbili. Nisingaliweza kubeba zile barafu za koni, kwa hiyo ningalizila. Ndipo ningenunua peremende kali za senti mbili, ingalikuwa karibu nusu pauni ya vitu hivyo. Naye Schimpff alivitengeneza hivyo. Nami ningeingia mle, na kukaa kitako nikimtazama William S. Hart.

69 Na huyu jamaa mdogo huyu, mwenye umri mkubwa kidogo kuliko mimi, alikuwa ameshikwa na ugonjwa fulani, hata wataalamu maarufu watano wa Louisville walimwepa tu, akiwa na uzito wa ratili arobaini na tano, alikuwa anakufa. Bibi Morgan alikuwa akimuuguza. Naye alikuwa katika hali mahututi sana! Alikuwa na mambo mengi sana; mapafu yake yalikuwa yamekwisha, koo lake lilikuwa limekwisha. Mikono yake midogo ilikuwa yapata *unene* kama huu, naye alikuwa amelala pale, anakufa.

70 Na Bibi Morgan alilipwa aifanye ile kazi. Basi akamwambia, "Wakati mmoja nilikuwa mgonjwa wa kansa," naye akaanza kumsimulia.

71 Akasema, "Umesema nani, Billy Branham? Mbona," akasema, "nimemuuzia kwa wingi vifurushi vya peremende kali na barafu za koni." Akasema, "Sijui kama angekuja kuniombea?" Nami nikaenda kule kumwombea Junie Schimpff.

72 Na sasa kama ungetaka kuzungumza naye, ni duka la Schimpff la Peremende la hapa chini, papo hapo kwenye mlango wa pili, au mlango wa pili kutoka Jumba la Michezo ya Kuigiza la LeRose, huko chini barabarani. Duka la Schimpff la Peremende, nyote hapa mnajua mahali lilipo. Jamani, ni mojawapo ya maduka ya zamani sana hapa Jeffersonville.

73 Na alipokuwa amelala pale, akifa, huku wataalamu watano wanampa masaa tu ya kuishi. Ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI, "Hutakufa; bali utaniuzia tena peremende kali, penye ile kaunta." Muda mrefu . . .

74 Nilijua alipata afya, bali kwa muda mrefu nilikuwa nimesahau jambo hilo. Nami na mke wangu tulikuwa tunashuka kwenda kununua peremende, tulipofika hapa wakati wa Krismasi. Na jinsi gani, sijui, tuliwahi kuwazia duka la Schimpff's. Sababu, kwa kawaida, huenda hapa kwa baadhi ya haya maduka ya madawa na kuzichukua, lakini tulisimama mbele ya duka la Schimpff.

75 Nilipoingia ndani, dada yake alitazama, naye akasema, "Vema, Ndugu Branham." Akasema, "Unamkumbuka Junie?"

76 Nikasema, "Ndiyo." Na pale, jamaa mkubwa mno, mwenye nguvu, na alionekana mwenye afya.

77 Nami nikatembea hadi kwenye kaunta, nikaitazama, nikatazama chini namna *hii*. Nikasema, "Nitachukua ratili moja ya hizo peremende."

78 Naye akasema, “Ndiyo, bwana.” Basi, dada yake alikuwa akimngojea mke wangu. Na, kwa hiyo, yeye akazitoa.

79 Nami nikasema, “Nilizoea kuzila, muda mrefu uliopita, hapa kwenye maonyesha ya sinema,” huku nimeinamisha chini kichwa changu.

Naye akasema, “Ndiyo,” kasema, “watoto wengi huzinunua hizo.”

“Wao bado wananunua,” nikasema.

Akasema, “Baba yangu alizitengeneza hizo, akabuni njia ya kuzitayarisha.”

Nikasema, “Ninazipenda kweli.”

80 Basi, baada ya kuzifunga na kunikabidhi, kasema, “Kuna kitu kingine?”

Nami nikasema, “Sijui,” nami nikainuka. Lo, jamani!

Akasema, “Ndugu Branham!”

81 Nikasema, “Hizi hapa zile peremende kali, ambazo, nilikwambia, ‘BWANA ASEMA HIVI,’ yapata miaka mitano iliyopita.”

82 Akasema, “Ndugu Branham, nimeponywa kabisa, hakuna dalili hata moja. Nina ugumu kidogo wa kusikia katika sikio moja.” Nadhani ana umri wa kwenye miaka hamsini. Akasema, “Nina ugumu kidogo wa kusikia katika sikio moja, kwa sababu walinipa dawa nyingi sana ya kuua viini vya magonjwa nilipokuwa kule.” Neema ya ajabu ya Yesu Kristo!

83 Sasa sina muda mwingi wa kutosha sasa kusema jambo jingine, bali na—na—nataka kutoa tamshi hili.

84 Ni wangapi wanakumbuka kuhusu wale kindi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sawa. Hilo lilikuwa Andiko la lililotatiza, maishani mwangu, kwamba kamwe siku—sikuweza kulielewa hilo.

85 Na kulikuwa na jingine lililonitatiza, ilikuwa ni ambapo Musa aliweza kumwambia Mungu njia bora kuliko Mungu alivyojua jinsi ya kufanya cho chote, wakati Musa aliposema, “Watu watasema, ‘Mungu Wenu aliweza kuwatoa, bali hakuweza kuwalinda,’” naye Musa akajitupa mwenyewe katika pengo. Kisha baadaye niligundua kwamba, Musa, huyo alikuwa Kristo ndani ya Musa, akisimama kwa ajili ya watu. Mnaona?

86 Kwa hiyo basi juu ya Andiko hili, ambalo kamwe nisingelihubiri juu yake, “Kama ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka’”. Nanyi mnajua kile kisa, kwa hiyo nitalipita hilo. Basi, ijapokuwa kidogo sikujua hilo lilikuwa linaelekeza wapi. Nami nafikiri ya kwamba Ndugu Woods na Ndugu Fred, na hao wengine, wako hapa jengoni, ambao walikuwapo wakati hilo lilipotukia, au mara tu baada ya hilo kutukia pale.

87 Na Ndugu Rodney na Ndugu Charlie, kutoka kule chini Kentucky, kaka ya Dada Wood na hao wengine walikuwapo wakati lilipotukia huko Kentucky, ambayo ilikuwa mara ya pili kutukia. Kunena tu vikaumbika, vitu ambavyo havikuwako. Unaona? Kunena, wakati wote, na kuyaunga mkono Maandiko, kutia moyo.

88 Mara ya tatu ilipotukia ilikuwa Hattie Wright. Je, Hattie yuko hapa usiku wa leo? Huyo ni nanii wa Edith. . . Wangapi wanamjua Hattie Wright? Mimi na Ndugu Woods tulikuwa tumeketi pale wakati lilipotukia, na wakati Roho Mtakatifu aliposema, "Mpe anachohitaji," nasi tulikuwa tukizungumza kuhusu jambo hilo, jinsi hao kindi walivyotokea.

89 Ndipo nikasema, "Ni, jambo pekee ni kwamba, Yeye ni Yehova-Yire. Wakati tu Ibrahimu alipohitaji kondoo dume, Mungu alimtoa kondoo huyo dume. Naye alitoa wale kindi. Yeye anaweza kunena tu kindi akaumbika, kwa sababu Yeye ni muumbaji, kama vile tu Yeye alivyoweza kumnena yule kondoo dume. Ibrahamu kamwe hakuwahi kuomba huyo. Alikuwa anakwenda tu kutenda hilo, lakini ilionyesha kwamba Yohava-Yire alikuwa pale."

90 Niliposema hilo, maskini mwanamke mnyenyekevu. . . Kwa mara ya kwanza hili lilipowahi kutukia, ule Mvuto wa Tatu, kwa mwanadamu, ilikuwa ni kwa maskini, mwanamke mnyenyekevu.

91 Huyo, akipata yapata dola mia mbili kwa mwaka, kwa riziki yake, zote alizopata kutoka katika shamba lake dogo. Mume wake amefariki; watoto wawili ambao walikuwa wamegeuka wakawa wajeuri. Naye akaja na kutoa dola ishirini, ya hizo, kwa ujenzi wa haya Maskani. Naye Meda alikuwa amenipa pesa asubuhi hiyo kwa ajili ya vyakula, dola ishirini, nami nilikuwa nakwenda kumrudishia hizo siku hiyo, wakati nilipokuwa ningali kule, ili kwamba isingelimbidi kuzilipa. Bali asingezipokea. Na wakati. . .

92 Alikuwa amekaa nyuma kwenye kona, na wakati niliposema, "Jambo pekee nijualo, ni kwamba, Yeye bado ni Yehova-Yire."

93 Ndipo maskini Hattie akasema neno sahihi. Akasema, "Hiyo si kitu ila Kweli."

94 Na wakati aliposema hilo, Ndugu Banks Woods hapa ni mmoja aliyekuwapo, hicho chumba kilisikika kama kilikuwa kinaporomoka. Ndipo Roho Mtakatifu akasema, Sauti ile ile ambayo ilinena kuhusu wale kindi, kasema, "Mpe anachoomba."

95 Nami nikasema, "Dada Hattie, kama shahidi mbele za Mungu, jambo ndilo hili. Basi, kama kuna mashaka yo yote niani mwako, wewe omba kile unachotaka, na kama hakiwekwi pajani mwako, basi mimi ni nabii wa uongo."

96 Akasema, "Ndugu Branham." Kila mtu alikuwa analia. Kasema "Niombe nini?"

97 Nikasema, "Wewe ni maskini, nawe unaishi kwenye kile kilima kule, bila pesa; unaweza kuomba hizo. Unaye maskini dada mlemavu amekaa hapa, Edith, ambaye tulimwombea, kwa miaka mingi; unaweza kuomba kuponywa kwake." Nikasema, "Baba yako na mama ni wazee na wamekongeka; unaweza kuomba kwa ajili yao. Lo lote utakaloomba, Dada Hattie, ona basi kama kitatukia au la, sasa hivi." Nami nikasema, "Yeye hivi punde ameniambia, Sauti ile ile, kasema, 'Mpe anachoomba.'"

98 Naye akatazama kila mahali, kasema, "Niseme nini, Ndugu Branham?"

99 Nikasema, "Sema kile ambacho ni shauku yako. Waza kuhusu shauku yako iliyo kuu kabisa, na sema hiyo."

100 Na wavulana wake walikuwa hata wanachekacheka kifichifichi na kucheka. Naye akasema, "Shauku kuu kabisa niliyo nayo ni ya wokovu wa wanangu wawili."

101 Nikasema, "Nakupa hao, katika Jina la Yesu Kristo," na hao pale hao wakaenda.

102 Nao wamekuwa waaminifu katika kanisa hili, kwenye ushirika, hao jamaa wadogo wakiketi pale wakitawadhana miguu na watu wazima, na mambo kama hayo. Sisi sote ni mashahidi wa hilo.

103 Alikuwa na chaguo halisi. Mama yake hana budi kufa, na yeye pia, wao wote. Bali alichoomba kitakuwa cha Milele, na wokovu wa watoto wake. Hiyo ilikuwa mara ya tatu lilipotukia.

104 Mara ya nne lilipotukia, nimeelezea hilo hapa mara ya mwisho niliyokuwa hapa, ilikuwa juu kule mlimani ambapo dhoruba ile ilikuwa inanguruma. Ni wangapi walisikia jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, nyinyi nyote. Vema. Ambapo ile dhoruba ilikuwa ikinguruma. Na Mungu akiwa Hakimu wangu nikisimama hapa, nikitelemka mlimani wakati . . .

105 David Wood, yuko hapa mahali fulani, nadhani, alinitengenezea sambusa, nayo ilikuwa nzuri hasa! Nafikiri alikuwa akijaribu kujilipizia kizazi kwa ajili ya ile niliyomtengenezea baba yake, miaka michache iliyopita. Alikuwa na mlo wa nyama mbalimbali, na—na nyama na kila kitu vimechanganywa pamoja. Nami niliiweka ndani ya shati langu, kisha kukanyesha, ndipo nikaipata tu kuwa bonge moja kubwa lililolowa maji.

106 Nami nilikuwa nikitelemka mlimani. Kulikuwa na dhoruba kubwa, hata nisingaliweza kuona mkono wangu mbele yangu, ilikuwa vigumu. Nami najua, jambo moja tu, unageuzwa, sababu huo upepo unavurumisha tu.

Sasa kuna mashahidi hapa, kwa jambo hilo.

107 Mmoja wao ni mmoja wa mashemasi wetu waaminifu, ambaye ni Ndugu Wheeler. Uko hapa, Ndugu Wheeler? Yuko wapi? Ndiyo, papa hapa, Ndugu Wheeler.

108 Ndugu Mann, mhubiri wa Kimethodisiti kutoka New Albany. Yeye yuko, Ndugu Mann, humu ndani usiku huu? Sijui kama yuko au la.

109 Ndugu Banks Woods. Uko hapa, Ndugu Banks? Yuko kwenye chumba cha kurekodia. Sawa. Na—na David Woods.

110 Na Ndugu Evans alikuwa hapa, naamini. Hilo ni kweli, Ndugu Evans? Ndugu Evans, anayesimama kuegemea ukuta, alikuweko.

111 Na jinsi walivyokuwa wametangaza kwa siku kadha, siku mbili kabla ya hapo, "Tufani kali ya theluji ilikuwa inaikumba nchi."

112 Ndugu Tom Simpson yuko hapa usiku wa leo. Alipokuwa akishuka kuja kutoka Canada, walimwomba kupita kando ya pale sababu yeye asingaliweza kupitia mle, "Tufani ya theluji ilikuwa inakuja." Ndugu Tom, uko hapa? Uko wapi? Yuko hapa, ameketi papa hapa.

Na hapo mawingu yakaja juu. Nami nikasema, "Ndugu . . . "

113 Kila mtu akitoka mbio. Hapakuwa na mtu nyuma kule, katika idadi ya watu mia na kitu nyuma kule, hapakuwa na mtu nyuma kule isipokuwa kundi letu dogo na yule cowboy, yule mpanda farasi. Nasi tulikuwa tukae.

114 Nilimpigia simu Dada Evans, nikamwambia ampigie mke wangu simu na kumwambia amwambie Tony, "Kama sikutoka, amtafute mtu mwingine aongoze mktutano wa kifunguakinywa kwa ajili ya Wafanya Biashara."

115 Na juu kule mlimani si—siku hiyo, nilisema, "Sasa wakati hiyo, kwanza mvua kidogo itakapoanza, au cho chote, kimbilieni kambini." Nikasema, "Katika dakika kumi au kumi na tano hamwezi kuona mikono yenu mbele yenu, kwa mojawapo ya hizo tufani, nayo itafunika futi ishirini za theluji katika muda mdogo tu, katika mlima."

116 Na hivyo ndivyo watu, mliyasoma katika gazeti, jinsi walivyo nyuma kule na kuangamia, na kila kitu. Bali sisi tulijua jinsi ya kutoka, nao walijua mahali tulipokuwa, na kwa hiyo tulisikia tukiongozwa kukaa.

117 Na kwa hiyo juu kule mlimani, wakati hiyo tufani ya theluji ilipoanza, nilianza kutelemka chini. Nami nilikuwa karibu yapata nusu maili kutoka mahali nilipoanzia, ndipo Sauti ya Mungu ikasema, "Geuka urudi nyuma."

118 Nami nikarudi kama Yeye alivyoniambia, baada ya kungoja kwa kitambo na kula sambusa ile ambayo David alinipa, kisha nikarudi juu kule nikaketi chini.

119 Na nilipokuwa nimeketi pale, na huo upepo ukitikisa na kuvuma, vilele vya miti vikiegemea kando, na mvua ya theluji na theluji vikipeperushwa namna hiyo, Sauti ikasema, “Mimi ni Mungu wa uumbaji.”

120 Nikainua macho yangu, nami nikawaza, “Hiyo ilikuwa wapi? Huo ulikuwa upepo, labda.”

121 Yeye akasema, “Niliumba mbingu na nchi. Nilituliza zile pepo zenye nguvu juu ya bahari,” na akaendelea kunena.

Niliruka juu na kuvua kofia yangu.

122 Ndipo Yeye akasema, “Iambie tu dhoruba, nayo itakoma. Cho chote usemacho, hicho ndicho kitakachotukia.”

123 Nami nikasema, “Dhoruba, koma. Nawe, jua, waka kama kawaida kwa siku nne, hadi tutakapokuwa tumetoka hapa.”

124 Kabla sijamaliza kusema hayo, ile mvua ya theluji, na theluji na kila kitu kilisimama. Katika dakika moja au mbili, jua kali lilikuwa linawaka mgongoni mwangu. Niliona zile pepo zinavuma namna *hii*, zikarudi kutoka Kaskazini, zikishuka. . .Namaanisha kutoka Mashariki, zikija kutoka Mashariki. Zilikuwa zinakuja kutoka Magharibi, pepo zilibadilika na kurudi *hivi*. Na yale mawingu, kama kitu cha siri, yakiinuka juu angani, na jua lilikuwa linawaka katika dakika chache.

125 Kisha Bwana Yesu akanena nami baadaye kidogo, kuhusu mke wangu kule chini, kama mnavyojua, kuhusu mahali nilipokwenda juu kule. Sijawahi kamwe kuwa nyumbani kwenye sikukuu bado, na ni miaka ishirini na miwili tangu tufunge ndoa. Sikukuu ya kwanza, ile ya kwanza, arusi yetu, mbona, nilimpeleka katika safari ya kuwinda. Sababu, nisingaliweza kugharimia ile ziara ya kuwinda, na—na—na kwenda katika fungate, pia, kwa hiyo kwa namna fulani nili—niliziweka zote pamoja. Na kwa hiyo, basi, basi nimekuwa nikiwinda tangu wakati huo. Nami nilijisikia kwamba hivyo ndivyo nilivyomtendea.

Naam, hiyo ilikuwa mara ya nne jambo hilo lilipotukia.

126 Sasa hapa kuna jambo fulani na—nataka kusema, nami ni lazima niseme kweli kabisa. Yapata miaka kumi na sita iliyopita nilikuwa California pamoja na Ndugu John Sharrit, nami nilikuwa na mkutano. Ndipo mimi na Meda, na Ndugu Sharrit na Dada Sharrit, na wengineo, tulikuwa tukikaa kwenye hoteli. Na mtu mmoja anayeitwa Paul Melikian, ambaye alisimama mumu humu katika Masikani hii mara nyingi; yeye ni Muamenia tajiri. Basi mkewe alikuwa amezaa mtoto huko Fresno, California, mahali walipoishi; nao walikuwa wamekuja kule, akashuka akaja na mkewe, kisha akanipigia simu pale hotelini, akasema, “Naweza kumleta mke wangu huko, Ndugu Branham?”

Nikasema, "Naam, unaweza." Siku ya pili, nilikuwa nikienda Catalina.

127 Kwa hiyo akashuka akaja pamoja na mkewe, na yule bibi alikuwa mgonjwa sana! Naye alionekana . . . Nikasema, "Weka mkono wako juu ya wangu, Dada Melikian," nikasema, "tutaona kama Bwana atatwambia." Na mara alipoweka mikono yake juu yangu, nikasema, "Loo, ni kuvilia miguu."

Yeye akasema, "Sionekani kama nina dalili yo yote."

128 Nikasema, "Wewe subiri." Katika siku mbili, walikuwa wakimfanyia matibabu kwa ugonjwa wa kuvilia miguu.

129 Kama maskini Jimmy Poole hapa, mtoto wake mchanga. Juzijuzi alikuja na huo ugonjwa wa moyo, ndivyo walivyodhania, nao ulikuwa ugonjwa wa pumu. Nami nikaweka mkono wangu juu yake. Nikasema, "Mtazameni kwa muda wa siku chache; yeye ana surua. Inaanza kumshika. Hiyo ni homa." Nilikutana naye jana usiku. Yeye akasema ameshikwa, mwili mzima, na surua. Unaona?

130 Basi, nilikuwa nikizungumza na Dada Melikian, kwa mkono. Yeye alisema, "Hilo ni jambo la kushangaza, kuangalia hilo, Ndugu Branham." Akasema, "Je, inatenda kazi kwa kila mkono?"

131 Nikasema, "Vema, kama mgonjwa ana kasoro." Nikasema, "Sasa hapa, nitawekelea mkono wangu," wengi wenu mlisimama na kutazama hilo, nalo halikutendeka. Nikasema, "Hapa, hakuna kasoro yo yote kwa mke wangu, akaweka mkono wake . . . "

132 "Tazama hapa, mpenzi, weka mkono wako juu ya wangu." Yeye amekaa pale, mke wangu. Akaweka mkono wake juu ya wangu. Mara tu ilipotendeka, nikasema, "Una uvimbe kwenye kifuko cha kushoto cha mayai. Una shida ya kike."

Kisha akasema, "Sisikii tofauti yo yote."

133 Nikasema, "Lakini unao." Becky alikuwa na umri wa miaka miwili. Binti yangu ambaye ndiyo kwanza apige kinanda, muda kitambo uliopita, alikuwa na umri wa miaka miwili.

134 Miaka miwili zaidi, Sara akajitokeza, na wakati . . . Alimzaa kwa kufanyiwa upasuaji. Nami nilimwomba Daktari Dillman, daktari wetu chini kule—kule Corydon, kwamba, "Ukishamfanyia upasuaji, tazama kile kifuko cha kushoto cha mayai," naye alifanya hivyo.

Akasema, "Hakuna kasoro, ambayo niliona." Nikaweka mkono wangu; nao ulikuwa bado upo.

135 Miaka minne baadaye akaja Joseph. Nilimwomba atazame tena. "Hakuna kasoro, kama nilivyoona." Nikaweka mkono wangu; bado ulikuwapo. Basi tukasahau hilo.

136 Sasa hili ni jambo ambalo yanibidi kusema. Sipendi kulisema, bali yapasa kuleta ile kweli, mnaona, na hiyo ndiyo mnayotaka. Sikuzote sema kweli, haidhuru kitakachotukia.

Miaka ilikuwa imepita, hatukuwa kamwe tumeuona.

137 Nami nasema hili, siyo kwa sababu amekaa pale, kwa sababu mimi hulisema wakati yeye hayupo. Nanyi mnajua hivyo. Siamini kungeweza kuwe na mke bora ulimwenguni kuliko mke wangu, nami natumaini sikuzote atadumu hivyo. Nami nataka kuwa mume mwaminifu, nami natumaini ya kwamba kila kijana mwanaume aliye katika jengo hili, wakati atakapooa, atapata mke kama mke wangu. Sijui ni kwa muda gani tutaishi namna hiyo, bali natumaini ni siku zetu zote zilizosalia duniani. Tumekuwa wenye furaha sana pamoja. Mungu ndiye aliyeniambia nimuoe.

138 Kwa wakati ule ule, bila yeye kujua, nilikuwa najaribu nisimuoe; siyo kwa sababu sikumpenda, bali kwa sababu sikudhani nilikuwa na uwezo wa kuyatunza maisha yake. Naye alikuwa mwanamke mzuri, nami sikustahili hilo kweli.

139 Basi yeye akatoka akaenda kuomba, akafungua Biblia. Nakisia . . . Alisema, “Bwana, kamwe sijawahi kufanya jambo hili hapo kabla, lakini nipe Andiko ambalo litanisaidia. Kama yanipasa kumsahau, sina budi kusahau jambo hili.” Kafungua Biblia . . .

140 Naye akatoka akaenda kwenye kibanda fulani kidogo akaomba. Na wakati alipoifungua ile Biblia, “Malaki 4. Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii kabla haijaja . . . ” Hiyo ilikuwa—hiyo ilikuwa miaka ishirini na kitu iliyopita, pasipokujua cho chote kuhusu huduma ya siku hii. Nami nilikuwa . . . nisingeweza ku-. . .

141 Nilikuwa nimejilaza chini mtoni kule. Naye akaniamsha—akaniamsha, usiku mmoja, nami nilimsikia Yeye akisimama pale karibu na mlango. Akasema, “Nenda ukamchukue, na arusi yenu itakuwa Oktoba hii ijayo, tarehe ishirini na tatu.” Na hilo ndilo hasa nililotenda. Nasi tumeishi kwa furaha. Kwa neema ya Mungu, hatujawahi kuwa na neno hata moja. Amekuwa kipenzi.

142 Siku moja niliingia ndani. Naye imemlazimu kuwalea watoto hawa peke yake; mimi huwa nikienda katika huduma. Siyo wanawake wengi wangevumilia hilo; mnajua hilo, ingekuwa vigumu kwao. Basi nikaingia ndani, naye akasema kitu fulani au kingine. Tunaye Joseph nyuma pale, naye ni . . . Yeye ni mvulana kwelikweli! Naye alisaidia kutia baadhi ya mvi katika kichwa cha mama yake, kama vile mimi nilivyofanya. Kwa hiyo alikuwa mvulana kwelikweli kwa jumla, naye alikuwa amefanya jambo baya sana. Nami nikamwambia . . . Yeye akaniambia, “Bill, mpige.”

Nikasema, “Sina ule ujasiri.” Unaona?

143 Naye akasema, “Ndiyo, kama ungelikuwa umeyavumilia hayo,” naye akaufunga mlango kwa nguvu papo hapo mbele yangu.

144 “Vema,” nikawaza, “hiyo ni sawa. Maskini jamaa huyo hakumaanisha hilo.”

145 Nilitoka nikaenda tu nje kuosha gari langu. Nami nilipotoka nje pale, Roho Mtakatifu hakulipenda hilo; akasema, “Nenda ukamwambie,” naamini ni Mambo ya Nyakati ya Pili, sura ya 22. Sikwenda. Nilifikiri, kwanza, nimewazia tu hilo. Niliendelea tu kuosha. Naye akasema tena, “Nenda ukamwambie asome hiki.”

146 Nami nikaingia ndani nikachukua Biblia, nikakisoma hicho. Ilikuwa ni ambapo Mu. . .au Miriamu, nabii wa kike, alimdhihaki ndugu yake, Musa, kwa kuoa msichana Mkushi, na Mungu hakulipenda hilo. Na Yeye alisema, “Ilikuwa ni bora kwa baba yake kumtemea mate usoni mwake, kuliko—kuliko—ku—kufanya jambo hilo.”

147 Basi, Miriam akashikwa na ukoma, mwili mzima. Na kwa hiyo Haruni akaja, akamwambia umbu lake, akasema. . .au akaja akamwambia ndugu yake, akasema, “Anakufa, kwa ukoma.”

148 Na kwa hiyo Musa akakimbia akaingia ndani kumwombea, madhabahuni. Na wakati alipofanya hivyo, ile Nguzo ya Moto ikashuka, Mungu. Yeye akasema, “Mwite yeye pamoja na Haruni, uwalete hapa.” Naye Haruni alikuwa katika jambo hilo, pia. Kwa hiyo akasema, “Waite waje hapa.”

149 Akasema, “Akiwapo mmoja miongoni mwenu,” Mungu akinena nao sasa, “ambaye ni wa kiroho, au nabii, Mimi Bwana nitajifunua Mwenyewe kwake. Mimi nitanena naye kwa maono, na kujifunua Mwenyewe kwake kwa ndoto, na—na kufunua ndoto, na kadhalika.” Akasema, “Bali mtumishi Wangu, Musa, hakuna mtu katika nchi kama yeye.” Yeye akasema, “Mimi nanena naye mdomo kwa sikio.” Akasema, “Hamkumwogopa Mungu?” Mnaona, Mungu hakupendezwa na jambo hilo.

150 Vema, nilipoona jambo hilo, nilikimbia ndani. Naye alikuwa katika chumba kingine. Nikapiga hodi mlangoni. Alikuwa amejifungia ndani. Nami nikamwambia nataka kuzungumza naye. Nami nikaingia mle ndani nikaanza kuzungumza naye, nikajaribu kumweleza ilivyokuwa. Nikasema, “Kipenzi, unajua jinsi ninavyokupenda, lakini Mungu hakufurahishwa na jambo hilo. Hukupaswa kusema hilo.” Mara baada ya hayo, akaanza kuwa na shida ubavuni mwake.

151 Tukampeleka kwa daktari hapa Louisville, Daktari Arthur Schoen, naye akagundua uvimbe kwenye kifuko cha kushoto cha mayai, ambao nilikuwa nimegundua miaka kumi na mitano au kumi na sita hapo kabla. “Uvimbe kwenye kifuko cha kushoto cha mayai, wapata ukubwa wa jozi.”

Nikasema, "Wasemaje, daktari?"

152 Akasema, "Hebu tuone kitakachotukia. Mrudishe tena baada ya miezi michache, yapata miezi miwili au kitu kama hicho."

153 Tukamrudisha. Ulikuwa umekua, kutoka jozi hadi yapata ukubwa wa limau. Kasema, "Afadhali utolewe; endapo utakuwa laini na wa kufisha."

154 Nami nikasema, "Naam, jamani," nikasema, tuna—tunakwenda Tucson. Bwana amenituma huko Tucson."

155 Yeye akamtuma kwa mtaalamu wa wanawake; yeye hakutaka hilo liwe mikononi mwake. Kwa hiyo hapana shaka alimweleza kuhusu huduma yangu, sababu yeye… Yule mwanamke mtaalamu wa wanawake alisema, "Utapaswa kutolewa." Kwa hiyo akasema…Tulimwambia tulikuwa tunakwenda huko—huko Tucson. Akasema, "Vema, ninaye mtaalamu kule, rafiki yangu mpendwa. Nilikuwa nikiishi Tucson." Akasema, "Nitawapeleka kwake."

156 Kwa hiyo akaandika hati na kuituma kwake, akasema, "Bibi Branham ni bibi mzuri," na kuendelea namna hiyo. Kasema…Akamtumia mchoro wa kuonyesha ukubwa wa ule uvimbe, na kadhalika. Ulikuwa umegeuka ukawa uvimbe wakati ule; na kasema jinsi ulivyokuwa mkubwa. Kisha kasema, "Najua…" Mnajua, alijua yeye…nafikiri yeye alidhani, aliniita "mponya wa Kiungu." Hivyo tu ndivyo yeye alivyojua jinsi ya kuliweka. Bali kasema, "Nimekubali kwamba—kwamba ungeweza kutolewa, nao unapaswa kutolewa. Kama hauna budi kutolewa, utoe."

157 Bali ilikuwa ni kujaribu imani yetu. Na mara kwa mara tuliomba. Na kadiri tulivyoomba, ndivyo huo uvimbe ulivyozidi kukua, hata ukafika mahali ambapo hata ulikuwa unatokeza nje katika ubavu wake. Hatukumwambia mtu; watu wachache hapa walijua hilo; tukijaribu kuona kile kingetukia. Ukazidi kukua.

Hatimaye, wakati niliposhuka nikaja kutoka Canada, kutoka mahali nilipoacha…

158 Bwana alinipa kuliongoza hilo kabila la Wahindi kwa Kristo. Ninarudi kwenda kuwabatiza, katika Jina la Bwana Yesu, majira haya ya Kuchipua, Bwana akipenda.

159 Basi, nikashuka nikaja, nao ulikuwa wakati wa kuondoka, nilipokuwa New York…au chini hapa kufanyiwa mwingine upasu…kufanyiwa ule upasuaji, au kuchunguzwa kwa mara ya mwisho. Nikaondoka nikaenda New York. Na wakati niliporudi, nikasimama humu, kisha nikapanda kwenda… Baada ya kuwa na mkutano hapa, ule mkutano wa mwisho, nilipanda nikaenda kule nikampigia simu kutoka kwa Ndugu Wood.

160 Naye akasema, "Bill, siwezi hata kuvumilia nguo zangu kuugusa." Ulikuwa umetokeza tu sana namna *hii* katika ubavu

wake wakati huo. Na mguu wake upande huo, angeweza tu kuchechemea, na lile lilikuwa juma baya sana alilowahi kuwa nalo. Sasa ameketi pale, ananisikiliza. Juma baya mno alilowahi kuwa nalo. Naye akasema, "Yanipasa niende, kesho kutwa, kwa ajili ya uchunguzi huo."

161 Nikawaza, "Ee Mungu, kama wataukata wautoe, hilo litatuzuia tusiende nyumbani Krismasi, nami nilikwisha waambia watu nitakuwa kule." Nami nikasema, "Ni wakati wa jinsi gani! Loo, jamani!" Niliwaza.

162 "Mwambie, kama atakufanyia upasuaji, vema, 'Hebu na auahirishe kidogo, mpaka baada ya Krismasi'"

163 Kisha nikawa ninawaza, "Unaweza ukawa ni wa kufisha mauti." Na nyuma *hapa*, mnajua, hicho ni kitu kibaya, unakimbilia nyuma katika figo. Kama moja kwa moja, utafikia madhara, utakuua. Basi nikawaza, "Naweza kufanya nini?"

Ndipo Meda akasema, "Vema, basi, nipigie simu," kasema.

164 Ile siku ambayo nilifika Shreveport, ambayo ingekuwa kesho yake, wakati nilipofika Shreveport, ilimbidi kwenda akafanyiwe uchunguzi. Na kwa hiyo alikwenda kwenye...Bibi Norman alikuwa anakwenda, Dada Norman; nyinyi nyote mnamjua, watu wanaokuja hapa katika Maskani. Alikuwa anakwenda naye, na kwa huyu mtaalamu. Na kwa hiyo akasema, "Ngoja mpaka uwe na usiku wako wa kwanza, hapo—hapo...na ndipo urudi." Sababu, ile tofauti, ni muda wa saa mbili. "Kisha nipigie simu wakati utakaporudi, baada ya mkutano, nitakwambia linalonipasa kutenda."

Nami nikasema, "Sawa." Kwa hiyo, nikaondoka nikaenda.

165 Basi asubuhi yake, kabla sijaondoka, nilikuwa nakwenda kuwachukua Billy na Loyce. Wote wawili wako hapa wameketi. Na sikuzote...

166 Tunacho kimeza kidogo cha kale pale ambacho Ndugu Palmer alitufunikia, hapa siyo muda mrefu uliopita, na sikuzote tunakizunguka kimeza kidogo hicho na kuomba, kila tunapo-...Ni cha kale cha aina ya Ottomani, aina hiyo, mwajua, mahali pa kuwekea miguu. Kila tunapozunguka pale na kuomba, wakati ninapokwenda katika mkutano, tunamwomba Mungu atusaidie.

167 Nami nilikuwa juu pale, siku chache, nami nilikuwa—nilikuwa mkiwa. Ile nyumba; watoto wamekwenda, naye amekwenda. Mnajua, wengi wenu mnajua ilinibidi kupitia hali hiyo wakati mmoja, kurudi kwenye nyumba tupu; ila tu, nilimzika mke huyo, Hope. Na sasa imerejea hali hiyo yote tena. Basi nikapiga magoti, nikawaza, "Vema, nitaomba kisha niende nikawachukue Billy na Loyce, tuondoke twende."

168 Kwa hiyo nilipopiga magoti niombe, nilisema, "Bwana, nina hamu ya kuwaona asubuhi ya leo, mahali hapa." Nikasema,

"Ninaomba kwamba Wewe utawasaidia na kuwabariki. Jalia turudi mahali hapa tena. Na sasa," nikasema, "wako nje kule kwa sababu Wewe ulinipeleka kule kwa ono, Nawe ulilitimiza. Sasa nataka kungoja, kuona yale utakayoniambia nitende baadaye." Nikasema, "Naomba kwa ajili ya . . . Mrehemu." Kisha nikasema, "Nisaidie katika mkutano chini kule." Na kisha nikaendelea . . . nikasema, "Bwana, usivache ulete madhara. Na hebu huyo daktari angojee hata baada ya tarehe ya kwanza ya mwaka, kuutoa. Na—nachukia kumwona yeye . . . "

169 Nikasema, "Bwana, hakumaanisha alilotenda asubuhi ile. Hakulimaanisha hilo." Nikasema, "Bwana, hata mara moja hajawahi kusema neno moja kuhusu mimi kwenda katika mikutano, nikikaa kwa miezi kadha, ama cho chote kile. Hata mara moja hajawahi kufungua mdomo wake kuhusu hilo. Sikuzote amepeleka nguo zangu kwa dobi, na kuosha mashati yangu, na aliweka kila kitu tayari kwa kwenda mkutanoni. Halafu, anashangaa jinsi gani anaweza kumtumikia Mungu."

170 Enyi wanawake, unapomtumikia mume wako, unamtumikia Mungu, bila shaka.

171 "Na sasa, basi wakati nilipoingia, nimechoka kabisa na kudhoofika, watu wakija kutoka kila mahali. Ingenibidi kwenda nje mahali fulani kwa safari ya kuvua samaki, au safari ya kuwinda. Mbona, wanawake wengi wangelipuka kwa jambo hilo. Yeye angefanya nini? Angetayarisha nguo zangu za kuwinda nipate kwenda; na kuniacha niende." Nikasema, "Bwana, yeye hakumaanisha hilo." Nami nikasema, "Ilimbidi afanyiwe upasuaji mara tatu, kwa sababu yeye alikuwa akizaa kwa kufanyiwa upasuaji." Nami nikasema ni- . . . "Bwana, nina—ninachukia kuona ikimbidi yeye kufanya hivyo tena."

172 Mara nikasikia kitu fulani chumbani. Nikainua macho yangu. Na Sauti ikasema, "Simama." Kasema, "Basi lo lote utakalosema, hivyo ndivyo itakavyokuwa."

173 Nilisubiri kwa dakika moja tu. Nikasema, "Kabla mkono wa daktari haujamgusa, mkono wa Mungu utaondoa ule uvimbe, na hata hautaonekana."

174 Hiyo ilimaliza mambo, kwangu mimi. Kamwe sikumpigia simu. Sisi tuliendelea na safari, nilikwenda nikamchukua Billy na Loyce, tukaenda Shreveport.

175 Usiku wa pili nilimpigia simu. Alikuwa mwenye furaha. Akasema, "Bill, nataka kukwambia!"

176 Sasa yeye yupo hapa, naye anaweza kuthibitisha hili. Ilimbidi kuchechemea alipoenda kule; alikwenda chumbani pamoja na nesi wa Bibi Norman, na kuvaa nguo zake kwa ajili ya . . . lile gauni, apate kufanyiwa uchunguzi. Daktari akatokea, naye ilikuwa ni vigumu kwake kupanda mezani; ule uvimbe ukining'inia juu pale, mkubwa sana. Na wakati yeye . . . Daktari aliingia naye akawa anazungumza naye. Ndipo akaja pale, apate

kufunua lile shuka amguse, na, punde tu kabla hajamgusa, ukaondoka.

177 Basi yule daktari hakujua ulikuwa upande gani. Akasema "Ngoja kidogo!" Akiwa na ile michoro ilichorwa na zile picha zote, na cho chote kile, yeye hakuweza kuona dalili moja ya huo. Alimfanyia uchunguzi, tena na tena. Akasema, "Huenda nisiweze kueleza jambo hili, bali, Bibi Branham, huo uvimbe haupo." Naye kamwe hajawahi kuwa na dalili moja ya huo, tangu wakati huo.

178 Ilikuwa ni nini? Tazama, sawasawa kabisa na ilivyosema, "Kabla mkono wa daktari haujaweza kuugusa." Sekunde moja, na mkono wake ungaliugusa. Jinsi lilivyo kamilifu Neno la Bwana!

179 Sasa, huyo hapo mke wangu, nasi sote tuko mbele za Mungu. Bali kabla mkono wa daktari haujaweza hata kuugusa mwili wake, akiwa njiani kuja kwake namna *hiyo*, jambo fulani lilitukia, ule uvimbe uliondoka. Nao hawakuweza, yeye—yeye alisema . . . Naamini ndivyo ilivyokuwa, sivyo, mpenzi? "Nataka kuwahakikishieni tena, Bibi Branham," (Sivyo, jinsi alivyosema? Hiyo ni kweli.) "kwamba huo uvimbe haupo. Huna uvimbe wo wote."

180 Ilikuwa ni nini? Sawasawa kabisa na Neno la Bwana, ambalo lilikuwa . . . ? . . . Amina. Hiyo ni mara ya tano. Tano ni namba ya neema, ni namba ya i-m-a-n-i, pia.

181 Hakuna shaka tena niani mwangu. Najua ule Mvuto wa Tatu ni nini, nami najua unayotenda. Basi iweni na kicho, kaeni kimya tu, ile saa itawadia hivi karibuni ambapo Mungu atatutendea mambo fulani makuu.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi mafupi.

182 Bwana Yesu, niliuona juu ya watu wengine, bali ulipokuja juu ya mke wangu wa thamani mwenyewe, ulikuwa nyumbani mwangu, wakati huo, Bwana. Niliutazama huo kwa macho yangu mwenyewe, nikaupapasa kwa mikono yangu mwenyewe. Na mimi . . . kumi na . . . miaka kumi na sita kabla ya huo, ulikuwa pia, Bwana, unajulikana na kufunuliwa na Wewe. Wakati cho chote kinaponenwa, ni lazima kitendeke. Wewe ulikuwa ukinionyesha mimi, Bwana, wakati huo, ya kwamba, hakikisho kwangu katika lile Wewe ulikuwa umetenda kwa ajili ya watu, na ungeacha mimi nijue, kusudi nipate kuwasadia wao. Wewe uliufanya kutimia nyumbani kwangu mwenyewe. Huo ulikuwa Mvuto wa Kwanza. Na sasa Mvuto wa Tatu ulithibitisha Mvuto wa Kwanza.

183 Tuna shukrani, Baba. Utusamehe makosa yetu. Sisi ni watu wadogo. Hatuna elimu, kwa kadiri, ni watu wasiojua kusoma. Bali tuna shukrani sana kwamba tunaye Mungu mkuu mwenye uwezo wote Ambaye hutulinda na kututunza, kwa

maana hatujui jinsi ya kujitunza wenyewe. Sisi tunajikabidhi wenyewe Kwako.

184 Sasa, Baba, naomba kwamba Wewe utanisaidia. Na katika huu Mvuto wa Tatu, jalia, Ee Bwana, kama vile umekuwa ukinena kwa miaka michache iliyopita kuhusu huo, ukiuonyesha huo juu ya . . . alama milimani, na kadhalika, na kuuanzisha huo. Basi, nilikuwa natazama kuona ulikuwa ni nini mpaka huo ulipothibitishwa kabisa. Sasa naomba, Baba, kwamba Wewe utanisaidia kuwa mnyenyekevu zaidi, kwa huu, kuliko ilivyokuwa hapo kabla, na Wewe upate utukufu. Kwa kuwa, juu ya mimbara ii hii, ambapo ule wa Kwanza ulisemwa, ule wa Pili, na sasa ule wa Tatu, na lile ulilosema limetimia hasa jinsi ulivyosema. Tunakuamini Wewe, Bwana Mungu.

185 Msaidie kila mmoja wetu kutupilia mbali kutokuamini kwetu na ushirikina wetu, tupate kusimama katika Uwepo wa Mungu aliye hai, tukijua kwamba, Mungu yeye yule aliyeondoa huo uvimbe kutoka kwa mke wangu ambaye yuko hapa ameketi sasa; imethibitishwa na baadhi ya wanasayansi wa madawa walio bora sana tulio nao nchini, ambao waliuchunguza, kisha wakauangalia, na na kuupiga picha; na sasa umeondoka. Wewe ni Mungu na hakuna mwingine zaidi Yako.

186 Nasi twakupenda Wewe kwa sababu Wewe ume—Wewe umetujalia kuwa watumishi Wako. Na naomba kwamba tukutumikie Wewe kwa unyenyekevu na heshima, siku zote za maisha yetu. Jalia hilo, Bwana. Hebu niweze, na jamaa yangu, na watu wote hawa, tuweze kuwa Mianga ing'aayo, chumvi yenye ladha ambayo ita . . . itaumba kiu ndani ya wengine, kumpenda huyu Yesu ambaye ametenda mengi sana kwa ajili yetu.

187 Sasa ninapofungua Neno, kusoma Hilo kwa ajili ya somo dogo, na kisha niwaombee wagonjwa, nisaidie, Bwana. Nena nasi, na uwaponye wagonjwa, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

188 Je, ninao muda kwa ajili tu ya . . . [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama nikiharakisha sana kwa ajili ya . . . fungu la maneno hapa, nataka nyinyi msome sasa, ama mwandike, au cho chote mnachotaka kufanya. Lile la kwanza linapatikana katika Kitabu cha Hesabu, 21:5 mpaka 19, nasi tunataka ku—kusoma hili.

> *Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri ili tufe jangwani? maana hapana chakula, wala hapana maji; na* nafsi *zetu zinakinai chakula hiki dhaifu,* chakula cha Malaika.
>
> *Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma; watu wengi wa Israeli wakafa.* Kwa hiyo Bwana . . .
>
> *Watu wakamwendea Musa, wakasema, . . .*

189 Kuungama! Tazama, "Tumefanya dhambi!" Mnaona, hilo ndilo jambo la kwanza kwa kuponya, kuungama kwanza.

> . . . *Tumefanya dhambi, kwa sababu*
>
> *tumemnung'unikia* BWANA, *na wewe; utuombee kwa BWANA,* yamkini *atatuondolea nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu.*
>
> *Bwana akamwambia Musa, Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti; na kwamba itakuwa, ita—itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo, ataishi.*
>
> *Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi.*

190 Sasa, pia, nataka kusoma Andiko kutoka Zakaria, sura ya 12, aya ya 10.

> *Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watanitazana mimi ambaye walimchoma, nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee, nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.*

191 Sasa kwa ajili ya somo, nitachukua hili: *Tazama Aliko Yesu*. Usiutazame ulimwengu, mtazame Yesu. Musa alitengeneza ile nyoka; na hapa nabii, baadaye, alikuwa akizungumza juu yake, nini kingetukia, kutazama aliko—aliko Yesu.

192 Biblia ilisema, katika Isaya 45:22. Tunaona ya kwamba Mungu alisema, "Nitazameni Mimi, enyi ncha zote za dunia." Na sasa wakati dunia itakapofikia mwisho wake, ama utaratibu wa ulimwengu ufikiapo mwisho wake, hebu watu wamtazame Yeye.

193 Sasa mnaweza kusema, "Tumesikia hili, kizazi baada ya kizazi. Tumesikia hili kwa muda mrefu." Hiyo ni kweli, na limehubiriwa kwa muda mrefu. Wahudumu wengi wamechukua somo lili hili, maelfu yao.

194 Bali hapa kuna jambo ninalotaka kuwaulizeni, usiku wa leo, kwa hizi dakika chache zijazo. Bali wakati unapotazama, swali ni—ni, unaona nini wakati unapotazama? Unaona nini wakati unapotazama? Hilo lategemea tu ni nini wewe unatafuta. Unaona? Sasa Yeye alisema, "Nitazameni Mimi, enyi ncha zote za dunia." Musa aliinua ile nyoka, na, kila aliyeitazama, aliponywa. Sasa, inategemea unatafuta nini.

195 Nimeona watu wakija kwenye mikutano, katika hii siku ya mwisho, wangeweza tu kukaa katika mkutano kwa karibu dakika moja au mbili. Hizo tu ndizo wangeweza kustahimili. Mnaona, wao wasingweza kustahimili.

196 Sitasahau kamwe, natumaini hili halimshutumu mtu ye yote kutoka Iowa, wakati nilipokuwa na mkutano kule Waterloo.

197 Ndugu Lee Vayle, alikuwa hapa asubuhi ya leo. Sijui kama yeye yuko hapa usiku wa leo au la. Uko hapa, Lee? Alikuwa hapa asubuhi hii. Ndiyo, nyuma huko kunakorekodiwa, nyuma hapa. Vema.

198 Mimi na Ndugu Lee tulifanya kila tulichoweza. Na tukawapa chama cha wahudumu kiamshakinywa, bure, tupate kushuka tuje tukazungumze nao. Ndugu Lee Vayle, bila shaka, ni mwanachuoni na—na Daktari wa Uungu, hata kweli aliistahili digrii yake. Na kwa hiyo nilijaribu kumfanya azungumze mbele ya hawa Waluteri, Wapresbiteri, na kadhalika, lakini akasema, "La, wanakutazamia wewe kufanya jambo hilo."

199 Vema, nilishuka nikaenda nikachukua somo langu, mbele ya hawa wahudumu, baada ya wao wote kumaliza kula. Nilichukua somo langu: *Sikuliasi Lile Ono La Mbinguni*. Mara tu niliposoma Andiko hilo, yapata watu wawili wakatazama, wakatokea mlangoni. Kwa hiyo nilipoanza kusema, "Kama vile Paulo katika siku yake, akiwa na huduma ya kipekee, na sasa anasimama mbele ya Agripa na kusema kwamba yeye hakuliasi hilo," yapata wengine wawili watatu zaidi wakasimama. Na wakati nilipofika mahali ambapo ningaliweza kusema jambo fulani kuhusu lile somo, kulikuwako tu na watu kama watatu wanne wameketi pale. Wote walikuwa wameamka wakaenda.

200 Sababu yake, ni, ni hii. Baadhi yao huja mkutanoni, wanaposikia kuhusu mwinjilisti, jinsi anavyovaa ina uhusiano fulani na watu. Kama havai nguo zinazosatahili, baadhi yao . . .

201 Nilimsikia msa—msaikolojia akisema, juzijuzi; Daktari Narramore, mtu mzuri, Mkristo, kipindi chake kiko KAIR kule, wakati wote. Alisema, "Njia ya kujua ya kwamba mtu fulani anarukwa na akili, ni wakati ambapo hakuvaa kulingana na cheo chake." Mnajua, jinsi anavyopaswa kuonekana mbele ya watu, hiyo ilikuwa ishara kwamba yeye alikuwa anarukwa akili.

202 Vema, basi, nimekuwa na kichaa maishani mwangu mwote basi, mnaona, maana mimi huvaa ovaroli na kila kitu, mnaona. Kwa hiyo, kulingana na cheo changu, ni lazima nivae kama kasisi, kwa maneno nmengine, ku—kuwa kasisi.

203 Sidhani Yesu alivaa kama kasisi. Alivaa kama mtu wa kawaida. Yeye alikwenda miongoni mwa watu, na haikuwa na uhusino wo wote na mavazi.

204 Bali hiyo tu ni, mnaona, jinsi hayo mawazo ya mwanadamu. Hilo hali-. . . Vipi kama mtu huyu, ama, nashangaa yule daktari angewazia nini juu ya jambo hili, wakati nabii fulani katika Biblia aliamriwa kuvua nguo zake na kutembea uchi mbele za watu? Yeye kweli angelikuwa na kichaa, sivyo sasa? Bali Mungu alimwambia afanye hivyo.

205 Mwingine alipaswa kulala kwa ubavu wake mia tatu na arobaini . . . Miezi, naamini ilikuwa hivyo, akilala kwa ubavu wake, upande mmoja; kisha akageuka upande mwingine. Na akala chungu cha dengu ambazo alikuwa amepika pale; ilimpasa aende akachemshe chakula hiki na kukitayarisha, pamoja, na kukila wakati ule wote; anaingiza mkono na kuchota konzi moja na kukila, huku amelala kwa ubavu, kwa ajili ya ishara. Mnaoana?

206 Loo, jinsi watu wanavyoweza kwenda mbali na, hasa, Neno la Mungu. Wanapata elimu sana mpaka wanajielimisha wenyewe wakajiondoa kwa Mungu. Wakati mtu anapozungumza kuhusu elimu yake, najua huo ndio umbali alioko kutoka kwa Mungu; mnaona, digrii ya udaktari. Sisemi hili dhidi ya Daktari Vayle, kwa sababu yeye si wa aina hiyo. Bali, kwa kawaida, mtu anapopata digrii ya udaktari, hilo tu lamaanisha, kwangu, yuko mbali kiasi hicho kutoka kwa Mungu, mnaona, isipokuwa awe anaweza kujishikilia mwenyewe kwenye Neno na kwa Mungu.

207 Basi, tunaona kwamba baadhi yao huja kusikia jinsi unavyozungumza, wanapokuja kutazama. Unanena kuhusu kuponya Kiungu na Bwana; kama mtu si mwenye akili maalum na wa asilia, watu hawawezi kustahimili kumsikia akitumia maneno kama "aiko, aimo," na—na maneno kama . . . Wao tu . . . Hawawezi. Wanafikiri kwamba hiyo ni mbali sana na Mungu.

208 Na wakati Yesu alizungumza lugha rahisi namna hiyo, mpaka, leo hii, imewafanya maprofesa kuchanganyikiwa, kwa maana wao wanajaribu kuifasiri kulingana na elimu na lugha ya kisasa, nayo ilikuwa lugha ya mitaani. Kwa hiyo . . .

209 Mbona, kuna tofauti kubwa sana hata hapa Marekani yetu! Nilipiga simu kutoka Florida, kwenda New York, na ilibidi kumpata mwanamke kutoka hapa, pia, pale Saint Louis, kufasiri kati ya huyu msichana wa kusini na msichana wa kaskazini. Hivyo ndivyo ilivyokuwa tofauti. Mnaona? Hakika.

210 Basi jambo lenyewe ni kwamba, ya kwamba watu huangalia mambo hayo, hotuba, badala ya Neno. Neno linapodhihirishwa ndiyo thibitisho kwamba Hilo ni kweli. Mnaona, Neno linapodhihirishwa! Wao kamwe hawaangalia Hilo. Yapasa uwe na ufahamu wa akili, kujua, uende seminari na kujifunza jinsi ya kuinama, jinsi ya kusimama mahali pamoja, na yote yale. Loo, hilo lingemkaba mhudumu, hata kufa, aliyejazwa kweli na Roho Mtakatifu. Mnaona? Basi, hiyo ni akili.

211 Na hiyo ndiyo njia ambayo hili taifa lote limepitia. Lina ufahamu wa kiakili wa Kristo. Hilo ndilo wanalotafuta. "Na kama Kristo akiwa ndani yako, huna budi kuwa mwanachuoni, huna budi kuwa mwenye akili," sababu hivyo ndivyo wao wanafikiri Kristo alivyo.

212 Na wakati mwingine, jambo jingine, wanaunda maoni yao wenyewe ya jinsi Yeye anapaswa kuwa, wazo lao wenyewe,

badala ya kuchukua kile Neno limesema. Hiyo ndiyo njia wao wanapotazama, na hata wanamwona Yesu Mwenyewe, wanashindwa kumtambua Yeye. Walitenda hivyo Siku ya Pentekoste. Walitenda hivyo wakati Hilo lilipokuwa katika mwili. Walitenda hilo wakati Yeye alipokuwa katika hori. Walitenda hilo wakati Yeye alipokuwa kwenye barabara za Yerusalemu. Walitenda hivyo alipokuwa msalabani. Naye alikuwa utimilifu wa hilo Neno. Na, hata hivyo, walikuwa na Masihi ukumbini akishuka kutoka Mbinguni, na cho chote kile, nao walikuwa wamekosea, kwa sababu ilikuwa ufahamu wao wa akili. Nao walishindwa kumwona Yeye, na, wakimtazama Yeye moja kwa moja. Ndivyo ilivyo leo!

213 Unaona nini unapotazama? Baadhi yao hutazama kuona, wanapomtazama Yeye, wanatazama kuona mwanzilishi maarufu wa kanisa mwenye akili nyingi, mtu fulani anayeweza kweli kutengeneza kanuni ya imani itakayowafanya watu wote kushawishiwa na kanuni hii ya imani, cho chote kile. Hilo ndilo wanalotazama wanapomwona Yeye.

214 Wengine wao hutazama kuona hadithi ya kubuniwa, kama vile Baba Krismasi, wanapotazama. Wao husoma Biblia, na kusema, "Haa, hicho ni kitu cha kubuniwa. Ni kitu fulani tu ambacho mtu aliandika. Hilo ndilo, wao, sababu wakati wao. . ." Oni unalochukua kuhusu Biblia, ndilo unalochukua kumhusu Yeye. Unaona?

215 Wengine hutazama kuona mtoto mchanga. Wengine hutazama na kuona su—sungura fulani ama Baba Krismasi fulani. Wengine hutazama kuona kitabu cha historia ambacho kilikuwa jana na sio leo.

Bali, swali ni, unaona nini unapotazama?

216 Wengi wenu, mnaodai kuwa na Roho Mtakatifu, mnatazama na kuona nafsi ya pili ya utatu. Ambapo, hata haijatajwa katika Biblia. Hakuna kitu kama hicho. Neno utatu hata halimo katika majalida ya Biblia. Lakini, hata hivyo, mnapomtazama Yesu, mnamfikiria Yeye kama nafsi ya tatu au nafsi ya pili ya utatu, na hiyo ndiyo sababu hamfiki po pote.

217 Mnajua Yeye alisema nini? "Mimi ni Mungu, na hakuna zaidi ya Mimi." Mnaona?

218 Inategemea unatazama nini. Kama unataka kuweka mvulana mdogo wa bahati, mzee mwenye ndevu, na kadhalika; kama hivyo ndivyo unavyomtazama Yesu kama kwamba ni mtu tofauti na Mungu, unatazama vibaya. Hulioni Hilo.

219 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa na jozi ya darubini. Nilikuwa najaribu kuangalia baadhi ya kulungu, au kulungu mmoja uwandani. Na mwanangu alikuwa akijaribu kunionyesha, naye ni kijana mdogo. Kwa hiyo alisema, "Chukua darubini hiyo, baba! Pale anasimama kulungu, hasa nje pale!"

Nikasema, "Naweza kumwona kwa macho yangu ya kawaida."

Akasema, "Chukua darubini hii."

220 Wakati nilipotazama, niliona yapata kulungu kumi, lakini darubini haikuwa inaona vizuri. Na wakati nilipozilenga vizuri, hao wote kumi wakawa mmoja.

221 Na kama utalenga akili yako kwenye Neno la Mungu, hao watatu watakuwa Mmoja. Mnaona? Lakini darubini yako ya kidini inalenga vibaya wakati unapojaribu kumfanya Yeye watatu. Yeye ni Mmoja. Unaona?

222 Bali inategemea wewe unatazama nini. Unaona nini unapotazama? Kumbuka, unaweza tu kumwona Yeye unapomtazama Yeye kupitia kwenye Neno. Huwezi kumtazama Yeye kupitia kitabu cha masomo. Huwezi kumtazama Yeye kupitia kanuni ya imani. Utaona miungu wawili ama watatu, na cho chote kile, katika kanuni hizo za imani. Bali mtazame Yeye kupitia katika Neno, nawe utaona kwamba Yeye ni "*Imanueli*, 'Mungu aliyefanyika mwili kati yetu.'" Yeye kasema, "Mimi ni Mungu, na zaidi yangu Mimi hakuna mwingine." Yeye ni Mungu.

223 Isaya alipotazama wakati mmoja, yule nabii, na wakati alipomwona Yesu...?...Somo langu ni, "kumtazama Yesu." *Tazama Aliko Yesu*. Wakati Isaya alitazama mbali na ulimwengu, apate kumwona Yeye, alisema, "Namwona Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele." Hilo ndilo Isaya alilotazama akaona.

224 Danieli, wakati mmoja, alikuwa akisimama wakati alipoona ule—ule mwisho wa falme za Mataifa. Aliona ile sanamu ambayo Nebukadreza alikuwa ameota. Aliona jinsi kila mmoja utakavyofuata mwingine, zilipoanza kuja. Na wakati alipotazama kuona yatakayotukia mwishoni, wakati alipomwona Yesu, Yeye alikuwa "Jiwe lililochongwa mlimani, bila kazi ya mikono," ambalo lilivunjavunja zile falme za Mataifa.

225 Nebukadreza alitupa wana watatu wa Kiebrania katika tanuru ya moto, ambao walimwamini Mungu na kusimama kwenye Neno Lake. Kama iliwapasa kufa kwa ajili ya Hilo, walikuwa watasimama, hata hivyo; jambo dogo tu, la kupiga magoti yao vingenevyo. Bali alipotazama aliko Yesu na akamwona, Yeye alikuwa "yule mtu wa nne" ambaye alikuwa katika tanuru iliyowaka moto, Naye aliweka joto lote mbali na watumishi Wake watiifu. Hilo ndilo Nebukadreza aliloona.

226 Ezekieli alitazama aliko apate kumwona Yeye siku moja, Naye alikuwa "Gurudumu katikati ya gurudumu," huko juu katikati ya anga. Yeye alikuwa Kikombe cha gurudumu, mahali ambapo kila taruma imefungiwa. Amina! Lile gurudumu kubwa lilikwenda kwa imani, bali lile Gurudumu dogo lilizunguka

kwa Nguvu za Bwana. Huyo ndiye Ezekieli aliyemwona wakati alipotazama aliko.

227 Yohana Mbatizaji alitazama aliko siku moja, na, alipofanya hivyo, aliona Hua; na Sauti, ikisema, “Huyu ni Mwanangu Mpendwa Ambaye Mimi ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Hilo ndilo yeye aliloona. Halafu, akamwona Yesu na Mungu wakiwa ni Mtu yule yule, sababu Roho alishuka kutoka Mbinguni kama Hua, akisema, “Huyu ni Mwanangu Mpendwa Ambaye Mimi napendezwa kukaa ndani Yake.” Hilo ndilo yeye aliloona. Angalia, Yeye hujitambulisha Mwenyewe kwa njia hiyo.

228 Nuhu, wakati alipotazama aliko apate kumwona Yeye, Nuhu aliona hukumu za haki za Mungu zikija juu ya watu wa ulimwengu huu ambao walikuwa wamelikataa Neno Lake. Hivyo ndivyo Nuhu alivyosema wakati alipotazama aliko.

229 Musa, wakati alipotazama aliko, aliona kijiti kikiwaka moto. Nguzo ya Moto ilikuwa imejirudisha Yenyewe kijitini, na, Musa aliposogea karibu Nayo, Yeye alisema, “Vua viatu vyako, kwa kuwa, ‘MIMI NIKO.’” Sasa, kama ungelipima neno hilo, “MIMI NIKO,” ni wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao. “MIMI NIKO,” Milele! Mnaona? “MIMI NIKO,” aliona yule “MIMI NIKO.” Hilo ndilo aliloona katika kijiti kilichowaka moto.

230 Israeli waliitazama nyoka ya shaba aliyotengeneza Musa, wakayaona mateso ya Kristo kwa ajili ya hukumu kwa ajili ya wagonjwa, kwa kuwa tunajua ya kwamba nyoka alinena juu ya Upatanisho.

231 Yesu alikuwa ule Upatanisho. “Kama Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa,” kwa kusudi lile lile. Mnaona? Kwa sababu gani? Walikuwa wametenda dhambi, wakawa wagonjwa; hiyo ilikuwa kwa ajili ya kuondoa dhambi zao na kwa ajili ya ugonjwa. Na hiyo ndiyo sababu, “Yesu alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Ondoa kuponya Kiungu kutoka kwa Kristo, unakatilia mbali nusu ya Upatanisho, katika sehemu mbili. Unaona?

232 Unaona nini Kwake unapotazama? Unaoana hilo? Je, unaona ya kwamba, “Yeye alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu; kwa mapigo Yake sisi tuliponywa”? Unapotazama aliko, unaweza kuona hilo, au unaweza tu kuona upande mmoja wa Upatanisho? Unaweza kuona pande mbili zake unapotazama?

Kama ukiutazama huo kupitia kanuni za imani, watakwambia, “Siku za kuponya zimepita.”

Bali kama ukiutazama kupitia kwenye Neno, utaona, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Unaona?

233 Wanafunzi walimtazama Yeye wakati walipokuwa katika bahari iliyochafuka, nao wakaona msaada pekee ambao ungaliweza kuwasaidia, ukija.

234 Martha alimtazama Yeye wakati wa mauti, naye akaona kwamba Yeye alikuwa "ufufuo na ule Uzima." Amina! Wakati wa mauti, Martha aliona, wakati alipomtazama Yeye . . . Yeye alikuwa amekataliwa na watu wake; alikuwa amegomewa; hata, alikuwa ametuma ujumbe akaitwe, Naye hakuja kwa kaka yake. Lakini hatimaye Yeye alipokuja, naye akaondoka akaenda akamsujudu kusudi apate kumtazama Yeye, aligundua kwamba Yeye alikuwa "ufufuo na Uzima pia." Amina!

235 Yairo alifanya jambo lile lile, mwamini wa kisirisiri; maskini Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbatisti, ambaye kweli aliamini, bali asingaliweza kusogea karibu, kwa sababu madhehebu yake yasingemruhusu, kwa sababu angelitengwa. Lakini binti yake mdogo wa pekee alilala mahututi, naye ilimbidi kwenda. Bali wakati alipompata Yeye, aligundua kwamba Yeye alikuwa ule ufufo na Uzima.

236 Wakati alipotuma ujumbe aitwe, tarishi alikuja akasema "Usimsumbue Mwalimu, kwa kuwa huyo msichana amekwisha kufa." Yeye . . . Na maskini moyo wake karibu uzimie.

237 Bali Yeye alisema, "Sikukwambia, 'Kama ukiamini tu, utaona Utukufu wa Mungu'?" Yairo aligundua kwamba Yeye angeweza kuwafufua wafu, wakati alipomtazama Yesu.

238 Wenye njaa walimtazama Yeye, wakapata chakula cha kuwasaidia maishani. Hiyo ilikuwa katika hali ya kawaida. Wenye njaa, kiroho, wanaweza kumtazama Yeye na wagundue kwamba Yeye ni Mkate wa Uzima.

239 Yule mwizi aliyekuwa anakufa alimtazama kuona kile angaliweza kuona, naye alipata, katika Yesu, msamaha wake. "Nikumbuke, Bwana, utakapokuja katika Ufalme Wako." Yesu akasema, "Leo utakuwa pamoja Nami paradiso." Hilo ndilo yeye aliloona katika saa ya kufa kwake.

240 Wagonjwa walimtazama Yeye, wakaona Mponya. Vipofu walitazama, nao waliweza kuona.

Inategemea unatazama nini sasa. Unatazama nini?

241 Petro na Nathanaeli walitazama, na kuona Neno lililoahidiwa la nabii wao, Musa, likidhihirishwa. "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi, nao watu watashikilia Kwake. Na wote wasiomwamini Yeye, na kumsikia huyo Nabii, watakatiliwa mbali na watu."

242 Na wakati Petro alipoingia katika Uwepo Wake, Yesu alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Alijua papo hapo, wakati alipomtazama Yesu kwa mara ya kwanza, ya kwamba hapo kulikuwa na utimilifu wa kile Neno la Mungu lilichosema Yeye angekuwa. Amina.

243 Sijui kama uliona kitu kile kile wakati ulipomtazama Yeye kwa mara ya kwanza? Sijui kama Neno lililoahidiwa lilijidhihirisha Lenyewe kwako wakati ulipomtazama Yeye?

244 Nathanaeli, mara tu alipokuja katika Uwepo wa Yesu, akiwa kidogo na mashaka...Tunaona kwamba Filipo alikuwa amekwenda na kumwambia, "Njoo, umwone Ambaye tumempata."

Ndipo Nathanaeli akaja, akasema, "Yeye ni Yupi?"

Akasema, "Labda ni yule pale juu anayewaombea wagonjwa."

245 Alijipenyeza hata akapata njia ya kumfikia apate kumtazama Yeye. Na wakati alipotazama, Yesu akasema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake." [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.]

Akasema "Rabi, umepataje kunitambua?"

246 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona."

247 Basi Nathanaeli aliona nini? Aligundua kwamba hapo alikuwapo Mfalme wa Israeli. Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli." Hilo ndilo aliloona wakati alipotazama. Alipata tafsiri ya Maandiko, yakifunuliwa mbele yake. Aliliona hilo, Andiko lile lile ambalo nabii Musa aliyepakwa mfuta alisema, "Yeye atakuwa nabii kama mimi."

248 Yule mwanamke kisimani, alitazama wakati mmoja, naye aliona nini? Alieleza hilo katika mji. Akasema, "Njoni, mtazame Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Wakati alipomtazama kwa mara yake ya kwanza Yesu Kristo, yeye alimwona Masihi.

249 Watu wanaweza kutazama kitu kile kile leo, na kukiita Hicho "kushirikiana mawazo." Wanakiita Hicho "ibada ya mizimu." Watakiita aina yo yote ya jina la pepo ambalo wanaweza kukiita Hicho, kwa sababu wao hawajui wanachotafuta. Amina. Wao hawaelewi. Wanatafuta kanuni ya imani. Wanamtafuta mtu mwenye akili apate kuliweka kanisa katika utaratibu. Wanatafuta washirika wengi zaidi, nao wanashindwa kumwona yule mbarikiwa Bwana Yesu Kristo katika Neno Lake lililotambulishwa. Sawa.

250 Inategemea unatafuta nini. Kama unatafuta kutimizwa kwa ile ahadi ya leo, utaiona. Bali, kama unamtafuta mtu mwenye akili, ama kitu fulani ambacho sikuzote wamekitafuta, mwanzilishi fulani maarufu, mwanahistoria fulani, mtu fulani mwingine, kitu fulani kingine, utashindwa kuliona Hilo. Bali unapomtazama Yeye kupitia kwenye Neno, Neno hutangaza kwamba Yeye ni Nani.

251 Yeye aliwasai watu wa siku Zake kufanya vile vile. Wao hawangeweza kumwona. Yeye akasema, "Enyi viongozi vipofu wa vipofu. Mnadai kwamba Musa ni nabii wenu. Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi. Musa aliandika habari Zangu Mimi." Nao walikuwa vipofu mno hata wasiweze kuona

Hilo. Wakilitazama moja kwa moja, nao walikuwa vipofu sana wasiweze kuliona Hilo.

252 Ninaumanisha huo "mng'ao," asubuhi hii, kwa dakika chache, mnaona. Wao wanatazama, na hawajui wanatafuta nini, kwa sababau wana wazo baya la kile wanachojaribu kutafuta. Ungejuaje kile ulichotaka kupata, kama hukujua ulichokuwa unatafuta?

253 Ungekwendaje kutafuta boga, nawe kamwe hujawahi kuwa moja na kamwe hujawahi kusikia habari zake? Ungekwendaje kutafuta tikiti maji, kama hujawahi kujua kuna kitu kama hicho, na sura yake? Mbona, ungeweza kuona beseni, na kufikiri hilo ni tikiti maji. Ungeweza kuona kitu kingine, ungeweza kuona tofali, na kufikiri hilo ni tikiti maji.

254 Bali yakupasa ujue unachotafuta. Na njia pekee ambayo utapata kujua kile unachokiendea, kile unachokitafuta; kama unamtafuta Yesu, utatazama kwenye Neno, kwa maana Yeye ni Neno. "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yachunguzeni Maandiko."

255 "Mnadai ninyi ni. . .ni waamini wa manabii, bali ninyi ni wa baba yenu ibilisi. Baba zenu, wanaodai; wakati Mungu alipowapelekea manabii, aliwatia katika kaburi. Wao—wao waliwaua hao manabii. Kila mmoja aliyekuja," Yesu alisema, "ni yupi mmoja kati yao ambaye baba zenu hawakumpiga kwa mawe? Na kazi za baba yenu mtazitenda." Amina! Mtu mwenye haki, mtu mtakatifu, mtu ambaye usingeweza kumwelekezea kidole, na hata hivyo Yeye aliwaita hao "majoka na mashetani." Unaona?

256 Unatafuta nini? Kama unamtafuta mtu fulani mtawa? Watu wengine wanafikiri ya kwamba ati kwa sababu Roho Mtakatifu angetenda kazi kupitia kwako, ungepaswa kuwa jamaa fulani mrefu, na mtawa, ambaye huenda kila mahali na hata hakuna. . .Huyo si Roho Mtakatifu. Mungu hatendi kazi kupitia kwa malaika kama hao, au wanaodhaniwa kuwa. Mungu hutenda kazi kupitia mwanadamu. Biblia ilisema, "Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi," bali usingaliweza kuwa pamoja naye isipokuwa umwone Yesu.

257 Petro na Yohana, penye lango liitwalo Mzuri. Na wakati walipowavuta juu kule kuhusu kuponywa huyo mtu, "Wao walikuwa wametambua kwamba walikuwa wasio na elimu, wasio na maarifa, bali wao pia walitambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu," mnaona, kwa sababu Uhai Wake ulikuwa ukionekana kupitia kwao.

Sasa, inategemea wewe unatafuta nini.

258 Yule mwanamke alikuwa amesoma Biblia. Yeye alijua Masihi yuaja, naye alijua huyo Masihi angetenda nini. Mara tu Yesu alipomwambia, "Niletee maji ninywe."

Akasema, "Siyo desturi." Yeye ni mtu wa kawaida tu.

259 Sasa, kama Yeye alikuwa amekaa pale amevaa kilemba kikubwa mno, na aina zote za mapambo, ya—ya mtu fulani mtakatifu, mbona, yule mwanamke angalisema, "Vema, huyo hapo kuhani," na kuendelea. Au, "Huyo hapo ni aina fulani ya mwalimu," na kuendelea.

260 Mhudumu, ye yote yule; niliona mtu akija kula, leo, mahali nilipoenda kula. Na jamaa huyo akaingia, ali—alikuwa amevaa misalaba ya kutosha na kadhalika; ni jambo jema wakati mwingine hao watu wawe na vitu hivyo. Nafikiri yakupasa kuishi maisha. Haikubidi uwe na mavazi mengi ya kikasisi, kuthibitisha wewe ni nani. Wakati mwingine wanakunywa, na kufanya ghasia nyingi sana, na kuvuta sigara, na kila kitu, hawana budi kuvaa mavazi ya kasisi kusudi hata ijulikane kama wao ni wahudumu au la. Hiyo ni kweli.

261 Nawaambieni, mavazi ya ukasisi ya mtu kuvaa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huo utakutambulisha ya kuwa uko pamoja na Yesu...?...Hiyo ni kweli.

262 Basi, tunaona, hilo lategemea wewe unatafuta nini. Mtu mwenye mavazi mazuri, nadhifu, namna ya kilemba; hutamwona Yeye kamwe, kwa sababu Yeye alikuwa mtu wa kawaida tu. Mungu hujihughulisha na mwanadamu. Yesu alikuwa mwanadamu; Mungu alikuwa katika huyo mwanadamu, Naye alikuwa Mungu.

263 Sasa, tunaona ya kwamba huyu mwanamke, wakati alipoona hii ishara ya ajabu, kwamba Yeye aliweza kumwambia yale aliyokuwa amekosea, au kilichokuwa moyoni mwake, alijua papo hapo kwamba huyo alikuwa Masihi. Kwa hiyo, wakati alipomtazama Yesu, alimwona Masihi.

264 Masihi, kazi za Masihi zilikuwa nini? Angejua siri ya moyoni. Hilo limekupata sawasawa? Sijui kama mtaelewa. Kama mngemtafuta Yeye, usiku wa leo, mngetazamia nini? Yeye angekuwa yeye yule. Masihi ni Neno, Neno! Na Biblia ilisema, katika Waebrania sura ya 4, ya kwamba, "Neno la Mungu li hai, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, lakata hata kugawanya mfupa, tena li jepesi kuyatambua mawazo yaliyo moyoni."

265 Na wakati alipojua ya kwamba Masihi alikuwa awe hilo Neno lililodhihirishwa, na aliweza kumwambia kasoro yake, alijua huyo alikuwa ni Masihi. Siyo jinsi Yeye alivyovaa, siyo kiasi cha elimu aliyokuwa nayo Yeye; bali, kwa ishara ambayo Yeye alimwonyesha, Yeye alikuwa Masihi. Wakati alipomwona Yesu, alimwona Masihi; Mungu ndani ya Mtu, kama ilivyoahidiwa kwa huo wakati uliotiwa mafuta.

266 Bali unajua nini? Wengi, wa nyakati zizo hizo ambazo nimewazungumzia, kamwe hawakuona jambo hilo. Wengi wao hawakuliona. Vivyo hivyo leo. Wengi hawakumtambua Musa. Wengi hawakumtambua Eliya. Wengi hawakumta-...

Wao hawawatambui mpaka wameondoka, ndipo wanatambua jambo hilo.

267 Yule asiyeamini aliona, katika siku za Nuhu, kipi tu ambacho kutokuamini hutazama? Nimewaambia ambacho mwamini aliona, sasa hebu tuone ambacho wasioamini waliona. Katika siku za Nuhu, wasioamini waliona—kuona nyuma kule walipotazama? Waliona "mshupavu wa dini, akiburuga kinachodhaniwa kuwa ni mashua." Hilo tu ndilo waliloona. "Mzee fulani kichaa mwenye sharafa ndefu zenye mvi, aliyerukwa na akili, na, dhidi ya uchunguzi na uthibitisho wa sayansi, kasema, 'Kuna maji juu kule.' Mbona, maskini mzee yule!" Walimwonea huruma. "Mpiteni; yeye, atatangazwa kuwa mwenda wazimu hivi karibuni. Amerukwa na akili."

268 Lakini alikuwa na Neno la Bwana. Alikuwa akijenga, juu yake, naye Mungu alikuwa akionyesha ushahidi kwamba ile gharika ilikuwa inakuja. Ilikuwa ni ishara kwao. Hao ambao hawakuamini habari za Nuhu walipotea katika giza, na kuishia mautini, majini, na kaburi la jehanum.

269 Farao, alitazama wakati mmoja. Aliona nini, aliona nini Farao? Aliona "mshupavu wa dini, anayedhaniwa kuwa nabii, mwenye yanayodhaniwa madai mengi ya ukombozi." Hilo tu ndilo waliloona; mfinyanga udongo, mtumwa akisimama miongoni mwa watu, na akisema yeye mwenyewe alitumwa na Mungu kutenda miujiza. Mbona, walifikiri yule mtu alikuwa amepoteza . . . Kasema, "Hebu, mwache apayukepayuke. Ata- . . . Watamtangaza kuwa 'mwenda wazimu,' baada ya muda kitambo."

270 Bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hao waamini, Haruni, Yoshua, na wengi wao, walimwona Mungu katika Musa. Na kazi za Mungu, Musa alizitenda, hiyo ndiyo sababu walijua Mungu alikuwa ndani yake. Wao walitazama wakamwona Mungu ndani ya Musa.

271 Yule tajiri alitazama akaona Yeye alikuwa Nani hasa. Unaona? Bali alikataa kumfuata Yeye, kwa sababu alipenda vitu vya ulimwengu, mno, asiweze kumfuata Yesu.

272 Ni matajiri wangapi watasikiliza kanda hii, wa aina hiyo! Si lazima uwe tu sikuzote ni tajiri wa fedha; la, unaweza kuwa tajiri wa tamaa, tajiri wa anasa za maisha haya. Ni wanaume wangapi, ni wasichana wadogo wangapi, na wavulana wadogo wangapi, hawataacha umaarufu wao wa umalkia wa uzinifu, au akina Ricky wenye zeze au gita, wakienda nje na kutumbuiza aina ya rumba, au aina ya dansi ambayo anaweza kucheza! Ni wangapi wao watadai utajiri wao wa umaarufu, na kukataa, wakati wanapoketi papa hapa katika mikutano na kuona Mkono wa Mungu ukitenda kazi na kulitangaza Neno Lake! Ni wangapi watafanya hilo!

273 Yeye alichagua madhehebu yake. Angaliweza kuishi kwake. “Yesu alikuwa shupavu wa dini,” kwa madhehebu yake. Kwa hiyo ilimpasa kuchukua aidha alilosema Yesu, au aidha ilimbidi kuchukua . . .

274 Mbona hakwenda kwa kuhani wake, na kusema, “Nifanye nini niupate Uzima wa Milele?” Alijua kuhani hakujua cho chote kuuhusu Huo.

Kwa hiyo alikuja kwa Yesu, na kusema, “Nifanye nini?”

275 Yesu akasema, “Shika zile amri.” Akalitupa moja kwa moja pajani mwake.

Akasema, “Nimeishatenda hili.”

276 Akasema, “Shika zile amri.” Kisha, alikuwa bado hana Uzima wa Milele, naye alijua hakuwa nao. Unaweza kushika amri zote, na usiwe na Uzima wa Milele, bado.

277 Kwa hiyo Yesu akasema, “Sasa, kama unataka kutenda lililo sahihi, nenda kauze ulivyo navyo, ukawape maskini. Uje, unifuate Mimi.

278 Lakini jambo hilo lilikuwa gumu mno kwake. Mnaona? Tuanaona ya kwamba yeye alitazama akaona Yeye ni Nani, lakini bado akakataa kulipokea. Basi tazamo lake la pili lilikuwa kuzimu, akiinua macho yake na kumwona Lazaro katika kifua cha Ibrahimu.

279 Pilato alitazama, wakati mmoja, wakati walipomleta Huyo. Alikuwa hajawahi kumwona Huyo kabla. Mikono Yake ilifungwa; damu ikitiririka mgongoni Mwake; taji ya miiba kichwani Mwake. Pilato alitazama, kisha akasadiki.

280 Kwa sababu, farasi alikuja akienda shoti barabarani, kisha mpanda farasi akaruka chini, akakimbia na kusema, “Hapa kuna, mkeo amekutumia barua.”

281 Naye akaitazama, na mkewe alisema, “Pilato, mume wangu mpendwa, usiwe na neno juu ya yule Mwenye haki, kwa sababu nimeteswa mengi katika ndoto kwa ajili Yake.”

282 Alitetemeka. Magoti yake yakagongana pamoja. Naye akasema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, kama Wewe ndiye yule Mfalme, mbona Wewe huneni waziwazi? Wewe ni Mfalme wa Israeli?”

Akasema, “Wewe umesema.”

Kasema, “Twambie ukweli.”

283 Akasema, “Kwa ajili hii nilizaliwa.” Na Pilato akastaajabu. Yeye . . .

284 Wote, kila mtu, alikuwa akibembeleza na kulia miguuni mwake. Akasema, “Mimi nina mamlaka ya kukuua Wewe, ama nina mamlaka ya kukufungua.”

285 Akasema, "Wewe huna mamlaka ya kitu, usingalipewa na Baba Yangu." Whiu!

286 Ndiyo Bwana, alikuwa amesadiki kwamba Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Alisadiki kabisa ya kwamba Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Hakika, alikuwa. Lakini (nini?) siasa zake na kupendwa na watu kulikuwa kukuu mno. Mnaona, alimkataa Yeye. Kupendwa kwake na watu kulikuwa kukuu mno. Siasa, cheo chake katika maisha, kilikuwa kikuu mno, asingeweza kumkubali huyu shupavu wa dini.

287 Sijui ni Pilato wangapi watakuwa wakisikiliza hili, ya kwamba nafasi yako katika madhehebu fulani itakuwa kuu mno, usiweze kumkubali Bwana Yesu aliye halisi akisimama mahali alipo leo.

Askari wa Kirumi, pale msalabani, alimtazama Yesu.

288 Baada ya dunia kupata msukosuko wa fadhaa, ikatetemeka hata mawe yakapasuka kutoka milimani. Nalo jua likatua mchana, likawa giza. Nyota hazikujitokeza kutoa mwanga wake. Kisha dunia ililipuka kwa miamba na tetemeko la ardhi. Na umeme wa mishazari ulitandaa mawinguni; na ukapasua pazia la hekalu kutoka juu mpaka chini. Na, watu wakikimbia na kupiga yowe, hawakujua yaliyokuwa yametukia.

289 Na askari huyo wa Kirumi aliyesaidia katika kumpigilia misumari Yeye pale, alikuwa amemchoma upanga katika moyo Wake, ndipo alitazama, lakini alikuwa amechelewa mno. Alitazama akaamini, lakini alikuwa amechelewa mno kuamini. Aliyokuwa ametenda yalitia muhuri maangamizi yake; alikuwa amechoma mkuki katika moyo wa Mwokozi. Alikuwa amechelewa mno.

290 Sijui ni Warumi wangapi leo wamefanya jambo lile lile leo, na watafanya jambo lili hilo. Huenda ukatazama, siku moja, bali yaweza kuonekana umechelewa mno. Wengi wa siku hizi watakuja siku hiyo na wawe namna ile ile. Wao wamejua.

291 Ndugu Woods hapa; jana. Nasema hili tu kwa sababu liko katika Ujumbe huu. Chini hapa kwenye Kampuni ya Slider, Mkatoliki wa Kirumi akiketi pale. Alishuka akaenda kuleta kokoto kwa ajili ya kanisa hapa, na, alipokwenda, alimwambia aliitaka kwa ajili ya mahali gani. Na yule Mkatoliki wa Kirumi akasema, "Huyo ni Ndugu Branham?"

"Naam."

292 Akasema, "Nitasema jambo moja; wakati anapoomba, Mungu hujibu." Mnaona?

293 Ajabu basi, wakijua jambo hilo, wakiona thibitisho kwamba kweli ni Injili, siyo mimi; mtu ye yote anayemwakilisha Kristo. Ni Neno tunalozungumza habari zake, siyo mtu.

294 Ninajaribu kusema nini? Ni jambo hili, ya kwamba, wanaona waziwazi Neno lililothibitishwa, kama vile Pilato na wengine

wote walivyofanya, kama yule askari wa Kirumi, lakini utangoja uchelewe sana kufanya jambo lo lote kuhusu hilo? Angalipaswa kutumia mkuki namna nyingine. Milango itafungwa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, halafu imechelewa mno. Yawezekana uamke asubuhi moja, na kusema, "Nakusudia kutoka katika mchafuko huu." Usingoje muda mrefu mno. Afadhali utazame uishi sasa.

295 Luther alitazama mbali na madhehebu ya Kikatoliki. Aliona nini? Nguzo ya Moto. Aliona kanisa linalojitegemea.

296 Wesley alitazama mbali na madhehebu ya Anglikana. Akaona jambo lile lile.

297 Wapentekoste walitazama mbali na madhehebu yote. Nao wakawa nini? Watu wakuu, wenye uwezo.

298 Kila mmoja wao alifanya nini? Wakati wale waanzilishi, Luther, na Wesley, na hao wengine, na wakati walipotazama na kuona waliloona na kuanza kutoka; watoto wao, wakija nyuma yao, walitazama nyuma mahali walikotoka, nje ya madhehebu, kisha wakalichukua wakalirudisha kundi hilo la watu kwenye mchafuko ule ule walikotoka.

299 Unatazama nini? Waanzilishi walitazama sawasawa. Bali watu, waliowafuata, walitazama nyuma mahali ambako waanzilishi walikotoka, na wakatenda hasa lile hasa waanzilishi walilokuwa wanapinga; Mpakwa mafuta wa Mungu.

300 Mnajua, sina budi kuharakisha, sababu ninao mstari wa maombi unaokuja, nami najua wengi wenu yawapasa kusafiri.

301 Siku moja nilitazama. Nikaliona Neno limefanyika mwili. Nilimwona yule Alfa na Omega. Kamwe sikuona watatu wo wote wale, wanne, au watano; nilimwona Mmoja. Nilimwona Yeye kama Mwokozi wangu. Nilimwona Yeye, Neno. Nilimwona Yeye, ile Nuru. Nilimwona Yeye, Mungu Mwenye Nguvu. Nilimwona Mungu ndani Yake. Niliona Nguzo ya Moto. Niliona, katika Yeye, kile hasa Biblia ilichosema Yeye alikuwa. Niliona ya kwamba Yeye alikuwa Alfa na Omega, na ya kwamba Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto. Yeye alikuwa yeye yule jana, leo, na hata milele. Niliona ya kwamba ile Nguzo ya Moto ilisema, ikamwambia Yohana, "Uwepo Wake usioshindwa." Kama alivyosema katika Yohana, pale, "Na Uwepo Wake usioshindwa kamwe hautakuacha kamwe." Ndugu, maoni yangu usiku huu, ni kuimba wimbo ule:

> "Tazama uishi," ndugu yangu, ishi,
> Mtazame Yesu hivi sasa upate kuishi;
> Kwa maana imeandikwa katika Neno Lake,
> haleluya!
> Ni kwamba tu "utazame upate kuishi."

302 Tazama! Unaona nini? Unaona ukombozi? Unaona kile Yeye alicho? Tazama kote katika Neno uone alichokuwa, kisha

utazame kote katika Neno lile lile na uone Yeye ni yeye yule leo kama alivyokuwa wakati ule. Yeye ni mfano kamili wa ile nyoka ya shaba jangwani, kwa sababu ile ile, dhambi na magonjwa.

303 Yuda alitazama, siku moja. Na baada ya kumtazama, baada ya kumtazama Yeye vizuri sana . . . Yeye alikuwa tu akiangalia ile hazina, hapo awali, ule mtungi wa pesa waliokuwa nao. Lakini siku moja wakati alipoangalia na kumwona Yesu, mnajua aliona nini? Alijiona ni mwenye hatia. Aliona kwamba yeye hafai kuishi, ndipo akajinyonga.

304 Asubuhi moja, moja ya asubuhi kuu sana katika historia ya wakati. Katika kufunga, ninasema jambo hili hivi. Kuna jambo fulani linalotendeka kule Yerusalemu, na mara moja kundi la askari wakashuka wakaja ge—gerezani. Naweza kusikia mlio wa ile—ile minyororo; nasikia mbururo wa mkuki barabarani.

305 Ni nani aliye kule nyuma? Baraba. Yeye yuko tayari kufa. Yeye ni mwizi. Hafai kitu. Ni mnyang'anyi. Ni muuaji. Hana budi kufa.

306 Muda si muda, yeye akasema, "Vema, yote yamekwisha kwangu. Nitauawa asubuhi."

307 Muda si muda, yule mlinzi akafungua mlango, "Toka nje, Baraba."

Akatoka nje akasema, "Vema, nadhani huu ndio mwisho wangu."

Akasema, "Baraba, wewe u huru kabisa."

"Ati nini? Ati niko nini? Mimi . . . "

"Huru kabisa! Uko huru," nilisema.

Kasema, "Nawezaje kuwa huru?"

308 Yeye akasema, "Vema, njoo hapa, Baraba, angalia *huku* juu. Unaona yule Mtu anayekufa pale juu? Yeye amepachukua mahali pako."

309 Sijui kama sisi sote, usiku huu, tungetazama tupate kuona kile alichoona Baraba, mtu fulani akipachukua mahali petu? "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake," mimi niliponywa, wewe uliponywa. Sijui kama, wenye hatia, ambao tunapaswa kuwa wagonjwa, tunaweza kuona katika Yeye ukombozi wetu? Ninyi ambao ingewapasa kwenda jehanum; oneni katika Yeye uhuru wenu, kibali chenu cha kwenda Mbinguni. Sijui kama mnaweza kuona kile Baraba alichoona siku ile.

310 Yeye alisema, "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona Mimi." Loo, enyi kanisa! Basi, kama Yeye alisema, "Ninyi mtaniona," ni thibitisho ya kwamba mnaweza kuangalia tena. "Mtaniona Mimi, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa

dahari." Lini? Mnamwonaje? Kwenye Neno. Yeye ni Neno. Angalia kwenye Neno uone ahadi ni nini, kwa maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

311 Alichokuwa wakati alipotembea Galilaya, ni jambo lile lile alilo huku Jeffersonville, jambo lili alilo kwenye Maskani ya Branham. Unaangalia uone nini, mwanzilishi, mtu wa kimadhehebu? Hutaona jambo hilo katika Yesu. Unatazama umwone mtu mkuu wa kikasisi? Hutaona jambo hilo katika Yesu. La. Unamwonaje Yesu? Kwenye Neno la Mungu likidhihirishwa, kwa maana Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo usiku wa leo, na atakuwa hivyo milele.

312 Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Nitaufupisha huu uwe mdogo.

313 Bwana Yesu, ni maombi yangu, jalia niangalie mbali na fadhaa za maisha. Bwana, na—najua sisi ni watu tu wa kawaida, wasio na elimu. Hatuna vitu vingi vya mali ya ulimwengu huu, bali tunakupenda, Bwana.

314 Nami nanena kwa niaba ya watu hawa. Wasingeketi mahali kama hapa, na kusukumana na kufinyana, na kila mahali katika umati wa watu, na kuketi, wakitoka jasho, na ka—katika joto, ama wakiganda kwa baridi, na kusimama katika. . .na kuja na watoto wao, wagonjwa na wanaoteseka, wakija huku; kama wanakuja hapa kuona kitu cho chote mbali na Wewe. Watu hao, Bwana, wasingekuja kamwe kumwona mwanadamu. Kuna watu wengi sana barabarani; wote wanafanana.

315 Bali wao wanakuja kumwona yule Mtu, yule Mtu wa Mungu, Yesu wa Nazareti wa mwili, akiwa Mungu. Sasa, Baba, umetwambia ya kwamba, "Bado kitambao kidogo, na ulimwengu haungekuona Wewe tena," hata waangalie namna gani, hawataliona. Bali Wewe ulisema, "Ninyi mtaniona Mimi," mwamini wa kweli, "maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Wewe umetuahidi sisi, kama tukiangalia, tungeona. Nami naomba, usiku wa leo, ya kwamba utalitimiza hilo Andiko kwetu tena usiku wa leo, tupate kuangalia na kumwona Yesu akijifunua Mwenyewe kwetu, katika njia ile ile Yeye aliyojifunua daima, akitimiza Neno Lake, tangu sasa, Bwana.

316 Nami nilitamka tamshi, kabla ya jambo hili, nami kweli niliyasema mambo haya kutoka moyoni mwangu, kuhusu ile Mivuto, Nawe uliniambia. Na sasa, hata lionekane kama fumbo namna gani, kama tu tungejifinya dhamiri yetu ya ndani, na kuona kwamba mambo hayo hayangeweza kutabiriwa, kikamilifu kama vile yanavyotabiriwa, isipokuwa yametoka kwa Mungu.

317 Tungewezaje kuona kitu hicho cha Kwanza kikitukia? Cha Pili kingeweza kutukia namna gani? Cha Tatu kingeweza

kutukia namna gani? Tungeweza kusimama namna gani hapa, miezi kadha kabla jambo hilo halijatukia, na kusema yatakayotukia kule Tucson? Na zile Muhuri Saba zingefunuliwa, na kuirudisha ile siri, na kuyafichua mambo ya Mungu yaliyofichwa, ambayo yamefichwa tangu mwanzo wa wakati. Na kuona hilo, yote mawili yamethibitishwa kisayansi, yakahakikishwa na kushuhudiwa!

318 Bwana, Wewe ndiwe kimbilio letu na nguvu zetu. Wewe ni yote tuliyo nayo. Nami nakushukuru, kwa kuwa, Bwana, mimi nikiwa ni sehemu ya uchumi huu Wako mkuu. Ninakushukuru, kwa kuwa mimi ni mshiriki wa Mwili Wako, pamoja na wengi hapa ambao ni washiriki wa Mwili huo, wengi kote ulimwenguni katika makanisa mbalimbali, ambao ni washiriki wa huo Mwili wa kisiri wa Kristo.

319 Kila wakati tunapoangalia, tunamwona Yeye! Tunamwona wakati ndege wanapoimba. Tunamwona wakati jua linapochomoza, ama wakati linapotua. Tunamsikia katika nyimbo. Tunamwangalia katika watu Wake. Tunamwona akithibitisha Neno Lake.

320 Ee Bwana, Wewe ni Mungu wetu. Tutakuita mapema. Wewe ndiwe Baba yetu uliye mwingi wa rehema. Tusamehe makosa yetu.

321 Bwana, tuko katika wakati wa mwisho. Naona milango itafungwa hivi karibuni, milango ya nafasi. Na wakati kungali ni mchana na ningali naweza kuingia katika baadhi ya mahali hapa, Bwana, nisaidie nipate kwenda. Ninazeeka; nipe nguvu. Rejesha ujana wangu, Bwana. Nisaidie, ili kwamba niweze kufanya jambo fulani kule nje, sasa, ambapo ninaungojea wakati huu mkuu ujao, ambao utakuwa hapa. Nisaidie, Bwana, ninapoenda kule nje, kusudi niweze, kwa njia fulani, kumshika yule Mzao wa mwisho aliyechaguliwa tangu zamani, jambo ambalo litamrudisha Bwana Yesu. Nisaidie, Ee Mungu!

322 Na iwapo ninaweka msingi ambamo mwingine atasimamia, jalia, Bwana, kwamba hivi karibuni itatendeka, Neno lipate kutimizwa.

323 Hamu ya mioyo yetu ni kuona Neno Lako likitimizwa. Tunakupenda. Tunakuamini Wewe. Katikati ya watu wasioamini, wanaoshuku, kizazi cha—cha—cha wale tulio nao leo, Bwana Mungu, tungali tunaamini ya kwamba Neno Lako halitashindwa kamwe. Tunaamini, ya kwamba, "Mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitashindwa kamwe." Tunasimama kishujaa kwa jambo Hilo.

324 Sasa, Baba, kwa hili kundi dogo ambalo limengoja. Kuna wengi walio wagonjwa humu ndani. Na huenda kuna wengi ambao hawajaokoka humu ndani. Watu ambao wameokoka, bali bado hawajajazwa na Roho Mtakatifu. Bwana Mungu, naomba ujitokeze, kwa Neno Lako la ahadi, ili kwamba watu waangalie

na kumwona Yesu, kisha wapige magoti na kuitoa mioyo yao Kwake. Jalia kwamba walio wagonjwa watazame na kuona ya kwamba haiwezekani kwa kitu kingine kufanya hivyo, ila Mungu tu, kwa maana ni ahadi ya Neno Lake.

325 Yale tumesema leo, Jumbe zote mbili, jalia yathibitishwe sasa. Yote yako mikononi Mwako, Bwana. Nami nimo mikononi Mwako. Na—na kusanyiko hili limo mikononi Mwako. Fanya kazi kupitia kwetu, Bwana, kuliheshimu Jina Lako lililo kuu. Ee Uliye wa Milele, tujalie hili kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

326 Najua kuna joto, nami nataka kujaribu kuwaombea wagonjwa sasa. Na kama tu mtanipa kama dakika kumi na tano hivi, dakika ishirini, sijui wametoa kadi ngapi, bali tutaanza tu na kuwaombea wagonjwa.

327 Sasa, Billy aliniambia ya kwamba alitoa, zilikuwa nini? [Mtu fulani anasema, "Moja hadi mia moja."—Mh.] Mia mo-. . . Ati nini, ati nini? [Mtu fulani anajibu.] Sawa. Vema, hebu na tuanze. Alisema alitoa kutoka moja hadi mia moja. Ni wangapi walio na kadi za maombi hapa? Inueni mikono yenu; kadi za maombi. Vema, kuna wengi kutosha. Tutajaribu kupata kila kitu tuwezacho, kama tukiweza. Naam, hatuwezi kuwa na upambanuzi kwa hao wote, mwajua, kwa hiyo tutaomba tu. Na, kila mtu, ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi, na hata hivyo mu wagonjwa? Inua mkono wako. Wengi.

328 Sasa, angalia. Ni nini? Sasa, najua, tunaweza tukawa tumechelewa kidogo kulingana na—na ratiba, kama dakika kumi na tano, bali nataka kusema jambo hili moja. Huenda ikawa ni tofauti kati ya, hapa, kuishi Milele Mbinguni ama Jehanum. Mnaona? Angalieni, iweni na kicho na mwe waangalifu, dakika moja, sikilizeni Neno, muone kama kwamba Yeye angali ni Kristo.

329 Naam, kila mtu hapa huenda ananijua. Na wengi wenu mimi siwajui, kwa maana siji hapa muda mrefu vya kutosha kuwajua. Na wengi wenu hukaa nje ya mji. Wangapi ni watu wanaokaa nje ya mji, inueni mikono yenu. Mnaona?

330 Naam, nilimuuliza mtu fulani anayekaa katikati ya mji, juzijuzi, nikasema, "Je, wewe huja kila mara?"

331 Kasema, "Hakuna haja ya sisi kuja." Kasema, "Kuna wengi sana wanaotoka nje ya mji, ambao wanakuja kule, hatuwezi kuingia." Mnaona?

332 Lakini hilo—hilo ni sawa. Tutapanga jinsi watakavyoingia. Njoni, hata hivyo. Angalia, wao walikuwa na nafasi kabla hujaipata. Naam.

333 Sasa kumbukeni, sasa, mimi ni ndugu yenu tu. Nina hakika mnaelewa jambo hilo. Mimi ni mwanadamu; Yeye ni Mungu. Bali Mungu tu ndiye anayeweza kutenda kazi, na daima ametenda

kazi, na alitenda kazi tu, kupitia kwa mwanadamu. Sasa tazama usiku wa leo, si kwangu mimi ama kwa mtu mwingine ye yote, bali mtazame Yesu Kristo.

334 Sasa angalia usiku wa leo kwenye Maandiko, kile yalichoahidi. Ni wangapi wenu. . .Naweza kutoa kila namna ya Maandiko, bali ni wangapi wataamini Waebrania 13:8, ya kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana. . ."? [Kusanyiko, "Amina."] Na ni wangapi wanaamini Yohana 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya"? ["Amina."] Mnaona? Ni wangapi wanaamini ya kwamba aliahidi ya kwamba mambo aliyotenda, katika njia ya "kupambanua mawazo ya moyo," yatarudi tena katika siku za mwisho kabla ya Kuja Kwake? ["Amina."] A-haa. Hakika. Sote tunajua jambo hilo. Sawa. Loo, ni mangapi zaidi, na mamia mangapi ya Maandiko, bali tunajua jambo hilo!

335 Sasa angalia. Usitazame kumwona mhudumu. Usitazame kumwona mchungaji. Tazama umwone Yesu. Usimwone mwanadamu; mwone Yesu. Unapotazama, mwone Yeye. Kama ningaliweza kukusaidia, ningefanya hivyo, bali siwezi. Siwezi kukusaidia; mimi ni ndugu yako tu. Bali, Yeye ni Bwana wako, mwangalie Yeye upate kuamini. Vema.

336 Sasa hebu tuanze na kadi nambari. . .Vema, tuanze kutoka namba moja. Ni wangapi. . .Namba moja, ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Inua mkono wako. Iko wapi? [Mtu fulani anasema, "Moja kwa moja nyuma kule."—Mh.] Unamaanisha ninino yako. . . ["Yeye anasimama."] Ilikuwa hiyo? Loo, nasikitika. Vema. Namba moja, njoo hapa, bibi, vema. . . Unataka kuwaleta upande upi, *huu*? Vema, njoo papa *hapa*, kama—kama ungeweza kutembea. Kama mtu ye yote ameitwa sasa, ambaye ni kilema, baadhi yetu na wakulete. Namba moja.

337 Namba mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? Inua mkono wako, upesi uwezavyo. Namba mbili, iko wapi? Siioni. Wapi? Nasikitika, si—siwezi. . . Papa hapa, bibi.

338 Namba tatu, utasimama, ama cho chote kile? Hiyo ni sawa, namba tatu.

339 Namba nne. Kadi ya maombi namba nne, waweza kuinua mkono wako? Iko wapi? Siioni. Kadi ya maombi namba nne. Unasemaje? Namba nne.

340 Namba tano. Ni nani aliye na namba tano, unaweza kuuinua mkono wako? Siioni. Namba tano.

341 Namba sita. Namba sita. Upesi, haraka sana, namba sita. Vema.

Saba. Wewe, saba? Sawa. Hiyo ni sawa.

342 Nane. Nane, upesi sana sasa. Inuka, upesi sana. Sawa, nane. Hiyo ni sawa, bwana.

Tisa. Tisa, iko wapi? Namba tisa. Vema.

Namba kumi. Kumi, vema, kumi, papa hapa. Kumi.

Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano.

343 Na hatutaita wengi sana, ili mpate... Mnaona, sababu ya kufanya jambo hili... Ni kadi tu iliyo na namba juu yake, mnaona, nawe unakuja tu kwa namba hii. Hiyo inawaweka kwenye mstari.

Kumi na tano. Kadi ya maombi kumi na tano. Vema.

344 Kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano.

345 Hebu waje, fanyeni mstari sasa, ishirini na tano, mpaka mtakapotengeneza mstari wenu. Simameni tu sasa kulingana na namba zenu. Hiyo ni sawa. Msije nyote pamoja. Pitieni upande huo mwingine, kama mkiweza, kama mko upande ule, njooni. Sasa ishirini no...

346 Tuliita ngapi, ishirini na tano? [Mtu fulani anasema, "Ishirini na tano."] Vema, hebu tusimame kwenye ishirini na tano, kwa dakika moja tu. Vema.

347 Sasa nasema, kama hamtaki kusimama kwa muda mrefu sana, mnapoona hao wakija, basi ingieni mara moja pamoja nao; ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba. Hivi, vema, ngoja, hebu mstari upungue kidogo, haitawabidi kusimama sana, kwa muda mrefu sana.

Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu.

348 Loo, marafiki, vipi sasa? Sasa tuko wapi? Sasa tuko mwi—mwisho. Tuko ambapo kitu fulani lazima kitendwe, kasema "ndiyo" au "siyo." Mungu hana budi apatikane kwamba ni wa kweli ama ni wa makosa.

349 Sasa, leo nimehubiri jumbe mbili, kwa nguvu, nikijaribu kuwaambieni Yeye ni nini, kuwaambia wakati unakwisha; alicho Yeye, alichokuwa Yeye. Na sasa tunapoangalia, usiku wa leo, hebu tumtazame Yeye.

350 Sasa, kila mtu, katika Jina la Bwana Yesu, na mkae kwenye viti vyenu sasa. Msisogee kila mahali. Ketini kimya hata mtakapoitwa. Hebu watoto wadogo...

351 Naam, kama ikitukia kwamba niseme, "Inamisheni vichwa," fanya hivyo upesi sana, mpenzi, maana vitu viovu vinatoka, kama vile kansa na magonjwa, na vinatoka vinaenda miongoni mwa watu, na kuwaingia wengine. Wote wanaoamini jambo hilo, na wanajua kwamba ni Maandiko, waseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tunaona, katika Biblia, ya kwamba pepo wachafu walimtoka mtu mmoja wakamwingia mwingine, walipotolewa. Nao wanajaribu kupata mahali.

352 Na ni mara ngapi tumeona jambo hilo mikutanoni! Watu wanakuja kwenye mkutano, wenye afya nzuri sana na wazima, wanaketi pale na kulaumu; na, siku moja ama mbili baadaye, wanakutwa ni vipofu kabisa, ama wameshikwa na kansa, wamepooza. Mnaona, kwa maana walikuwa wasioamini. Mimi siwajibiki kwao; ni kwa waamini tu. Wengi wao walienda hospitalini, miaka mingi iliyopita, na wangali kule, wengine wamekwenda makaburini mwao, kwa sababu tu ya kuwa na kiburi, kutokuamini.

353 Hakuna mahali pa wasioamini sasa. Ni mahali pa waamini. Mwaminini Mungu!

354 Baba wa Mbinguni, sasa mkutano ni Wako; umekuwa Wako, wakati wote. Sasa, naweza kunena juu ya Neno Lako; lakini sasa, tangu sasa, siwezi kulinena. Wewe ndiwe unayenena sasa, Bwana. Na ijulikane ya kwamba mtumishi Wako amewaambia Kweli. Jalia hawa watu hapa, labda wengi walio hapa ni wagonjwa, na hata hawatakuwa kwenye mstari wa maombi, bali Wewe ungali hapa, Bwana. Unaweza kuponya po pote pale, jinsi tu unavyoweza kuponya hapa kila mahali. Jalia Neno Lako lijulikane, katika Jina la Yesu, naomba. Amina.

355 Sasa kama naweza kupata usikivu wenu usiogawanyika kwa kitambo kidogo. Nataka kuangalia kwenye mstari huu wa maombi. Kweli siamini namjua mtu hata mmoja. Ninyi, mlio kwenye mtari huu wa maombi, nyote ni wageni kwangu, mnajua ya kwamba siwajui? Inueni mikono yenu kama ninyi ni wageni. Ni wageni. Ni wangapi huko wanajua ya kwamba sijui kitu juu yenu? Inueni mikono yenu, huko, mnaona. Hakika, asilimia tisini na tano ya watu hapa, siwajui. Hiyo ni kweli.

356 Sasa huyu hapa maskini mwanamke mmoja, sijapata kumwona maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Naam, huenda yeye yuko hapa kwa ajili ya ugonjwa. Huenda yeye yuko hapa. . . Labda amefanya kitu fulani. Labda yuko hapa kwa ajili ya fedha. Labda ni tatizo la kinyumbani. Labda yuko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui. Sina habari.

357 Bali hapa pana ile picha kabisa iliyo katika Yohana Mtakatifu, sura ya 4, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza. Na hapana shaka, ya kwamba, yule kijana mwanamke aliyekutana na Yesu, Yeye alikuwa na umri mkubwa kuliko huyo mwanamke, kwa sababu, "Yeye," wao walisema, "alionekana kuwa na umri wa miaka hamsini, ama zaidi ya hamsini," na labda kijana mwanamke mrembo aliyekuwa huko nje kisimani, alikuwa tu msichana mdogo. Na hapa tena, usiku huu, watu wawili wanakutana, kijana na mzee, bila mmoja kumjua mwingine.

358 Na sasa yeye anasimama pale. Kuna sababu ya yeye kuwa pale. Sijui. Anaweza kuwa amesimama pale, kama mdanganyifu. Anaweza kuwa amesimama pale, akisema kitu fulani, na huku si

kweli, kuona tu litakalotukia. Kama ndivyo ilivyo, hebu angalia linalotukia. Mnaona? Mnaona?

359 Sasa, mimi simjui huyu bibi; sijapata kumwona. Yeye aliinua tu mkono wake, kitambo kidogo kilichopita, ya kwamba mimi nilikuwa mgeni kwake. Nami nainua mkono wangu, yeye ni mgeni kwangu. Sijapata kumwona. Vema, sasa kama mimi . . .

360 Kama mwanamume tu, ingenipasa kusema, "Bibi, una tatizo gani? Unafanya nini hapa? Unataka nini?"

361 Naye angesema, "Bwana Branham, "Ni—niko hapa kwa sababu ni—nina ugonjwa wa ka—kansa. Nina ugonjwa wa TB. Nina uvimbe." Ama, "Sina pesa. Mimi . . . Mume wangu aliniacha." Ama, "Mimi sijaolewa, na mpenzi wangu alifanya kadha." Hana budi kuniambia.

362 "Vema," ningesema, "sawa, ni—ni—nitakuombea; na kukuwekelea mikono, na kusema, 'Bwana Mungu, mpe mwanamke huyu anayohitaji. Amina. Yesu, fanya jambo hilo!" Nimwache aondoke. Vema, nakisia, kama yeye angeamini hilo, angepata afya. Hilo ni sawa. Hiyo imekuwa huduma kwa miaka mingi, mingi sana.

363 Bali ilikuwa imeahidiwa, katika siku za mwisho, ya kwamba kama yule Malaika, Mungu, alivyokuwa akiishi katika mwili wa kibinadamu ambao ulitokea kabla tu ya Sodoma kuteketea, Naye akaketi huku mgongo Wake ukielekea kwenye hema alimokuwa Sara, na akamwambia Ibrahimu yale huyo mwanamke aliyokuwa anawazia humo hemani; Mungu, katika mwili wa kibinadamu, akivaa mavazi ya kibinadamu.

364 Na hivyo tu ndivyo Mungu anavyoweza kufanya leo, ni wakati anapoingia katika mwili wako, mnaona, ikionyesha ya kwamba Mungu angedhihirishwa katika mwili wa kibinadamu.

365 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Sisi tuna mjumbe, Billy Graham na hao wengine kule Sodoma, bali Kanisa lililoteuliwa lilipokea Ujumbe na mjumbe.

366 Sasa, kama maskini bibi huyu . . . kama Roho Mtakatifu . . . Sisemi atafanya hivyo, bali kama angekuja na kuniambia sababu gani umesimama hapa, ama—ama unachohitaji, ama kitu fulani ambacho umefanya, ama kitu fulani ambacho u karibu kufanya. Naam, ungejua ya kwamba chanzo chake hakina budi kuwa ni cha kimbinguni, maana sisi tumesimama hapa tu, mnaona. Hilo lingekuwa sawa, sivyo? Ndipo ungejua ilipaswa kutokana na chanzo cha kimbinguni. Na kama Biblia ilisema ya kwamba Yesu alifanya jambo lile lile, na aliahidi kulitenda tena katika siku za mwisho, basi mngeamini ilikuwa ni Yeye. Ni wangapi wanaamini jambo lile lile? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi mngemwona Yesu. Mngeliona Neno Lake.

Sasa mnasema, "Yeye ni Neno?"

367 Biblia inasema Yeye ni Neno. Na Biblia ilisema ya kwamba Neno hupambanua mawazo yaliyo moyoni. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi litakuwa ni Neno lililonenwa kupitia kwenye midomo ya mwanadamu, likipambanua mawazo.

368 Sasa, siwezi. Sina njia ya kufanya jambo hilo, mnaona, maana simjui; bali Yeye anamjua, Naye ni Neno.

369 Naye ndiye anayeweza kuzichukua roho zetu sisi wawili, kama yule mwanamke kisimani, pamoja Naye, na kuziunganisha; na kuondoka kwenda kunionyesha yeye yuko hapa kwa sababu gani, na yale aliyotenda, ama anachohitaji, ama cho chote kile. Ndipo ninaweza kulitamka na kulinena, halafu ni juu yake.

370 Sasa mnasema, "Ndugu Branham, unaweza kumponya?" La, la. Siwezi kufanya jambo hilo, Yeye amefanya jambo hilo tayari. Kwa mapigo Yake sisi tumeponywa.

371 Lakini jambo hilo ni la kuinua imani yake tu, kumfanya ajue, ya kwamba, kama Yeye anajua kile huyu mwamamke amekuwa na kile anachohitaji, Yeye anajua—anajua jinsi ya kumpa hicho na jinsi atakavyokuwa baadaye. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Naam, kila mtu anaamini hayo? ["Amina."]

372 Sasa iweni na kicho sana. Nanyi watu huko nje sasa, msio na kadi ya maombi, ombeni.

373 Sasa, kumbukeni, Yesu alipitia kwenye kundi moja siku moja, na maskini mwanamke mmoja akagusa vazi Lake. Basi akageuka, kasema, "Ni nani aliyenigusa?" Naye akatazama kila mahali kwenye lile kusanyiko hata akampata, ndipo akamwambia alikuwa anatokwa na damu. Na kutokwa kwake na damu kukakoma wakati huo. Mnaona?

374 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Yeye sasa ni "Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu." Sivyo?

375 Ninaangalia hapa kwa Ndugu Way, ameketi hapa karibu na mke wake. Hivi majuzi huyu mtu alikuwa amesimama hapa nilipokuwa ninahubiri, kama tu vile Paulo alivyokuwa akihubiri usiku kucha usiku mmoja, na mtu huyu akaanguka akafa mkutanoni. Kisha Roho Mtakatifu akamfufua tena. Yeye ni shahidi, mnaona, ya kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

376 Ni wangapi hawakuwa wamewahi kumwona Ndugu Way, na wangetaka kumwona; inueni mikono yenu, wale hawajawahi kumwona. Ndugu Way, ungetaka kusimama? Huyu hapa huyo mtu, alianguka akafa karibu na pale anapoketi sasa hivi. Huyu hapa mkewe, nesi aliyehitimu, akisimama pale pale. Hakuwa na

mpigo wa moyo, umekoma; macho yake yamerudi nyuma, naye alikuwa mweusi usoni; ugonjwa mbaya wa moyo.

377 Daktari alimwambia alikuwa na ugonjwa mbaya wa moyo. Lakini kabla ya hapo, nilikuwa nimeugundua katika upambanuzi, si muda mrefu uliopita, kisha nikamwambia alikuwa na ugonjwa mbaya wa moyo. Ndipo, mara, moyo wake ukakoma, naye akaanguka chini. Naye alikuwa hapo, amelala pale, ameaga dunia kabisa.

378 Hiyo ni kama mara sita au nane ambapo nimemwona Bwana Yesu akiwafufua wafu. Nimemwona Yeye akifanya hivyo, Naye anaweza kufanya jambo hilo usiku huu.

379 Sasa namchukua kila roho, humu ndani, chini ya mamlaka yangu, kwa utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Iweni na kicho. Tazameni.

380 Nataka kuzungumza nawe, bibi. Nilikuwa nikihubiri, mnaona. Na ili tu niipate roho yako, hivyo ndivyo ninavyofanya hasa. Unaona?

381 Kuna kitu fulani ndani yako, uhai fulani, la sivyo hungekuwa umesimama pale; ungekuwa tu umbo, lilokufa, na hungekuwa na uhai ndani yako. Lakini, kwa kuwa kuna uhai katika mwili huo, unakutawala. Unaona? Na sasa hata mawazo yako na kile unachofikiria, maneno unenayo, na kila kitu, ndiyo unayoishi kwayo. Unaona? Hivyo ndivyo ulivyo, ni maneno yako, mafikira yako, na vyo vyote ulivyo.

Naam, tuko, tuko hapa, tukiamini. Sasa Roho Mtakatifu . . .

Kama vile Yesu alivyomwambia yule mwanamke, “Nipe maji ninywe.”

382 Na, wakati alipoyaleta, alisema, “Mbona, Wewe, Wewe hupaswi kuniomba hayo. Mi—mimi ni Msamaria. Wewe ni . . . Wewe ni Myahudi. Hatuna desturi sisi kwa sisi, ha—hata kidogo, hatuzungumziani sisi kwa sisi.”

383 Sasa, lakini, bila shaka, sisi sote ni Mataifa. Na tunasimama hapa tukimwamini Mungu. Sasa, kama Roho Wake akija kwa njia yangu kwa kipawa, na anaweza kukwambia yale, ili kwamba ujue kama ni kweli ama si kweli, kwa maana umeishi sehemu hiyo ya maisha. Ndipo, una kipawa, kuamini jambo hilo. Nawe kama utaamini jambo hilo, Naye atakwambia jambo hilo, basi yote yamekwisha. Na itafanya kazi kwa kila mmoja hapa. Sasa, kila mtu na awe na kicho sana.

384 Na bibi huyu anasumbuliwa na kasoro fulani kooni mwake. Ni ugonjwa wa koo. Kama jambo hilo ni kweli, inua mkono wako. Naam, sijapata kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo lililomleta hapa, ili nipate kumwombea koo lake.

385 Sasa, papo hapo, mara niliposema jambo hilo, ama kabla tu sijalisema, yeye alikuwa . . . Alijua ya kwamba kulikuwa na Kitu

fulani karibu naye. Kitu fulani kilikuja karibu naye, wakati uo huo. Mliweza kuona msisimko juu yake, kama hali ya hisi nzuri hasa, ilimpata.

386 Nuru ile mnayoiona kwenye picha. Uko wapi, George? Hiyo Nuru iliyokuwa kwenye picha, inaning'inia moja kwa moja juu ya huyu mwanamke, sasa hivi. Mnaona, ni kiwango kingine. Yeye ni mwamini, si anayejifanya mwamini. Yeye ni mwamini.

387 Naam, na kwa kuwa wewe ni mwamini, unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, na nabii? Sina budi kuwa hivyo, nipate kujua jambo hilo. [Yule dada anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Unaamini Yeye anaweza kukuambia mambo mengine yaliyo moyoni mwako? ["Naam, bwana."] Vema.

388 Hapa kuna jambo lililo moyoni mwako. Ni mtu fulani unayemwombea; mtoto. Unaamini Yeye anaweza kuniambia ana kasoro gani? Ana viini. Sivyo? [Yule dada anasema, "Hiyo ni kweli. Naam."—Mh.] Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? ["Naam, bwana."] Wewe ni Bibi Walker. ["Sawa."] Hutoki hapa. ["La."] Umetoka Kusini. ["Sawa.] Georgia. ["Sawa."] Unaenda zako nyumbani, mzima. Yesu Kristo amekuponya pamoja na mtoto wako. Usifadhaike juu ya jambo hilo. Imekwisha. Mungu na akubariki, dada.

389 U hali gani? Sasa huyu hapa mwanamke mwingine. Simjui yeye, sijapata kumwona. Yeye ni mwanamke tu anayesimama pale. Sasa angalia, nimekuwa nikihubiri, kwa jumla, tangu yapata saa mbili, na ni saa nne sasa. Hayo ni masaa mawili nimekuwa hapa. Huo upambanuzi mmoja umenichosha zaidi ya masaa hayo mawili ya kuhubiri. Mnaona? Hiyo ni . . . Mnaona?

Mnasema, "Unataka kusema hivyo?" Loo, ndiyo.

390 Mwanamke yule aliyeugusa upindo wa vazi Lake. Yeye alisema, "Naona ya kuwa nguvu zimenitoka," nguvu. Sivyo? Hivyo ndivyo unavyofanya.

Naam, huyu papa hapa mwanamke ambaye sijamwona kamwe.

391 Billy alienda kule, kama uliona kitu fulani, akamchukua huyo mvulana tuliye naye hapa, George. Yeye ni mvulana wa Kibatisti. Nataka yeye aone ya kwamba kile tunachozungumzia ni Mungu. Baba yake ni, jamaa yake, ni watu wazuri. Wako kule Mexico, mmishenari, mtu mzuri. Na baba yake ni mgonjwa, pia. Ninamngojea tu yeye aje. Sasa angalia kwa makini, George.

392 Sasa, bibi huyu, si—si—simjui. Si—sijapata kumwona. Nadhani sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. [Yule dada anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hatufahamiani.

393 Lakini sasa, Roho Mtakatifu, utamu wa Yesu ukiweko, sisi sote tunashuhudia jambo hilo. Sasa kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani juu yako . . .

394 Sasa, kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, bali siwezi kufanya jambo ambalo Yeye amekwishatenda tayari. Jambo pekee ni kwamba, kama Yeye angekuwa amesimama hapa usiku huu huku amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, vema, sasa, Yeye—Yeye hangaliweza kukuponya, kwa maana amekwishafanya jambo hilo. "Kwa mapigo Yake sisi tumeponywa." Mnaona? Bali jambo tu ambalo angalifanya, kujitangaza kwa Neno aliloahidi, na kukufanya uone ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naye aliahidi kufanya jambo hilo.

395 Sasa kama Yeye atanitumia kukwambia uko hapa kwa sababu gani, utatumia imani uliyo nayo, katika Yeye, kuamini ya kwamba unapokea uliyoomba . . . ama yaliyokuleta hapa? Kwa moyo wako wote? [Yule dada anasema, "Ndiyo, nitafanya hivyo."] Sawa, Bwana na akujalie jambo hilo.

396 Naona bibi huyu ana kasoro fulani. Uchunguzi unaonyesha ya kwamba ni tu—tumbo lililopasuka. [Yule dada anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hiyo ni kweli. ["Hiyo ni kweli."] Ni kweli, naam, bwana, tumbo lililopasuka. ["Naam."] Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya mpasuko huo? ["Naam, bwana. Naamini yote ninayoweza kuamini."] Wewe, yote u—u- . . . ["Kwa moyo wangu wote."] Mungu akubariki. ["Mungu anaweza kuponya tumbo langu."]

397 Sasa, hutoki hapa. [Yule dada anasema, "La, bwana."—Mh.] Umejitolea sana upate kufika hapa. ["Naam, nimejitolea."] Ulijitolea. ["Mungu asifiwe!"] Naam. Naam. Umetoka Tennessee. [Naam, bwana."] Hiyo ni kweli. Bibi Hart. ["Hiyo ni kweli."] Rudi; usitie shaka. Utaponywa, kama unaweza kuamini.

398 U hali gani, bibi? Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. [Yule dada anasema, "Hiyo ni kweli."] Sijapata kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Huenda nimekuona, mahali fulani mkutanoni, nawe huenda umeniona, bali mimi sikujui. Mungu anakujua. Unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake, na neno ambalo nimehubiri ni Kweli? Vema, kwa kuwa mimi ni mgeni kwako; nalo Neno, ambalo nimehubiri, umeliamini.

399 Jambo pekee, ni kwamba, baadhi yao walikupa wewe kadi; aidha mmoja wa mabawabu, ama mwanangu, ama mtu fulani alikupa wewe kadi. Namba yako iliitwa, nawe uko hapa. Hilo tu ndilo ninalojua.

400 Bali wewe uko hapa, ukiugua ugonjwa wa fadhaa. Unakusumbua sana. Una mtu fulani pamoja nawe. Una mtu unayemwombea. Ni . . . mume wako. Naye ana tatizo la kiroho ambalo hawezi kulitatua. Kisha una mtoto mgonjwa, pia. Hutoki hapa, bali umetoka Kaskazini. Umetoka Canada, kutoka Alberta. Hiyo ni kweli. Wewe unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, na kuamini ya kwamba ninayokwambia ni Kweli, nenda

nyumbani na utapokea yale uliyo nayo. Naam. Amini. Mungu akubariki, bibi.

401 Mimi ni mgeni kwako. Wewe ni mgeni kwangu. Sikujui. Bali Mungu anakujua. Unaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake? [Yule dada anasema, "Ndiyo, naamini."] Kwa moyo wako wote? Sikujui, sijui kitu juu yako. Kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, lakini si—siwezi. ["Amina."] Mimi si mponya. Mimi ni mwanadamu tu. Bali Yeye ni Mungu. Nimetatanishwa kidogo, kwa maana kuna mwanamke mzee kidogo anayesimama kati yangu na wewe. Ni mtu fulani ambaye unamwombea. ["Naam."] Naam. Ni mama yako. ["Naam, ndivyo. Naam."] Naye huugua ugonjwa wa m—msukumo wa damu. ["Naam, anao."] Nawe una fi—figo lililoambukizwa. ["Naam, bwana."] Hiyo ni kweli. ["Hiyo ni kweli."] Unaamini jambo hilo? ["Naam, naamini."]

402 Mama yako hayuko hapa. [Yule dada anasema, "La."—Mh.] Bali ukienda kwake, chukua shali hiyo uliyojizungushia shingoni, ukaiweke juu ya mama yako, na usitie shaka, na huo msukumo wa damu utamwacha, na huko kuambukizwa kwako kutakwisha. Nenda zako, amini sasa.

403 Mnaamini sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa mioyo yenu yote? ["Amina."] Sasa, mnaona, ninaangalia kote mkutanoni, na inaonekana tu kana kwamba ku—kumeanza tu kuwa na ukungu, kama ukungu, huko nje. [Mahali patupu kwenye kanda.]

404 "Mambo haya nifanyayo mtayafanya pia." Yeye amefanya zaidi papa hapa, usiku wa leo, kuliko Yeye. . .ya namna hiyo, kuliko aliyofanya katika safari Yake nzima ya maisha. Hiyo ni kweli.

Sasa, bibi huyu mmoja hapa, kijana mwanamke. Simjui, yeye ni mgeni kwangu. Bali unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? [Yule dada anasema, "Naam."—Mh.] Sasa hebu kidogo.

405 Mtu amekuja mbele yangu, mtu fulani kwenye kusanyiko. Sasa hebu kidogo. Mtu fulani kwenye kusanyiko. Imeondoka hapa wakati huo tu; hiyo Nuru imeondoka hapa. Na kuna mtu aliyekuwa amesimama karibu Nayo, na mahali fulani kwenye kusanyiko. Usihofu tu; uwe na moyo wa ushujaa.

406 Hebu turudi tena tukamshughulikie huyo mwanamke. Sasa kama Bwana Mungu. . .Huyu ni wa sita saba, ama ye yote yule, ambaye amepitia mstarini, chini ya upambanuzi. Na kama Bwana Yesu atanifunulia, juu ya huyu mwanamke, kasoro yo yote aliyo nayo, hiyo ingewafanya wengine wenu kuamini kwa mioyo yenu yote? Mngemkubali Kristo kwa misingi hiyo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Mnaona? Wakati mmoja unapaswa kuthibitisha jambo hilo. Mara tatu ni uthibitisho. Na hii ni mara makumi ya maelfu, bila kukosea wakati mmoja.

407 Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mwanamume fulani. Nami namwona ameketi huku ameinamisha kichwa chake. Yeye anavuta sigara, nawe unaomba ya kwamba hizo sigara zimwache. Hiyo ni . . . Bwana Mungu na akujalie unaloomba, dada. Nenda zako, ukiamini kwa moyo wako wote, na tabia hiyo ya ibilisi na imwache mumeo, katika Jina la Bwana Yesu.

408 Shida yako iko mgongoni. Unaamini Mungu atafanya mzima? Unaamini? [Yule dada anasema, "Naamini."—Mh.] Vema. Nenda zako, useme, "Asante, Bwana."

409 Namjua mwanamke huyu, naamini ni binti wa Bibi Neece. Hiyo ni kweli? [Huyo dada anasema, "Naam."—Mh.] Nilifikiri ndiye. Mungu akubariki. Ile shida ya kale itakuacha sasa nawe unaweza kwenda na ukapate afya.

410 Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuiponya hiyo yabisi kavu na kukupa afya? Nenda zako ukamwambie unamwamini Yeye. Amini tu kwa moyo wako wote.

411 U hali gani, bwana? Unaamini Mungu anaweza kukuponya huo ugonjwa wa tumbo na kukufanya mzima? [Yule ndugu anasema, "Amini."—Mh.] Sawa, nenda zako basi, useme, "Namshukuru Bwana, sasa ni—nitapata afya." Nawe—nawe—nawe utapata afya.

412 Kisa kingine cha yabisi kavu, na umri, pia. Unaamini ya kwamba Mungu atakufanya mzima kama nikikuwekelea mikono? [Yule dada anasema, "Amefanya hivyo mara nyingi, kwa njia yako, kwa kuniwekelea mikono, ndugu."—Mh.] Mlisikia hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Bwana ambariki dada yangu, na ampe ukumbozi usiku huu tena. Amina. Mwamini Yeye tu.

413 Ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa tumbo. [Huyo dada anasema, "Naam."] Unaamini Mungu anaweza kuuponya? Sawa. Nenda zako, katika Jina la Bwana Yesu, na akufanye mzima.

414 U hali gani, ewe jamaa mdogo? Ugonjwa wa pumu. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya pumu? [Yule ndugu anasema, "Naam."] Nenda zako, amini hilo; Yeye atafanya hivyo. Vema.

415 Ugonjwa wa sukari. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuiponya damu yako na kukupa afya? Nenda zako, mwamini, Yeye atafanya jambo hilo, amini kwa moyo wako wote.

416 Vipi kama sikukwambia lo lote; nilikuwekelea mikono tu; unaamini Roho Mtakatifu yuko hapa kukupa afya? [Yule mgonjwa anasema, "Naam."] Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Njoo hapa. Katika jina la Yesu Kristo, na aondoke aende akaponywe. Amina.

417 Njoo, bibi. Kama sikusema kitu kwako, unaamini Mungu angekuponya na shida hiyo ya wanawa- . . . La, samahani, Yeye

tayari ameutaja. Nenda zako. Mungu akubariki. Nenda zako, ondoka uende, ukiamini, halafu, na upate afya.

418 Unaamini, bwana, kwa moyo wako wote? Mungu huponya ugonjwa wa moyo, sivyo? [Huyo ndugu anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Humpa mtu afya. Nina hakika Yeye hufanya hivyo.

419 yeye, Yeye ni Mungu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaamini kwa moyo wako wote? [Amine] Mwamini Mungu!

420 Baadhi ya watu hapa walifanya jambo fulani, dakika chache tu zilizopita. Nataka kuona hilo. Ilikuwa ni damu. Mtu fulani kama kwamba ni ajali, ama kitu fulani kilichotukia. Ilikuwa—ilikuwa ni kutokwa na damu. Ilikuwa mahali fulani. Mtu huyo alikuwa amesimama hapa; ndiyo kwanza niombe. Naam, ndivyo. Ni huyu mtu anayeke-. . . Naam, ni J.T. Parnell. Namjua huyu mvulana. Unatokwa na damu ndani, J.T. Unaamini Mungu atakufanya mzima? Vema, itakoma basi, kama ukiamini. Amini kwa moyo wako wote.

421 Maskini bibi anayeketi hapa, akiangalia toka upande mwingine, ameketi pale karibu na Ndugu Grimsley. Kuna Nuru iliyo karibu naye. Wewe, ukosi mdogo mweupe. Mary, sikujui, bali hilo ndilo jina lako. Unasumbuliwa na tatizo la kiroho, na pia wewe una wasiwasi sana. Sahau hayo; yote itakuwa sawa. Amini kwa moyo wako wote. Mwamini Mungu. Kama unaweza tu kuamini.

422 Maskini bibi huyu anayeketi moja kwa moja kule nyuma kwenye safu ya nyuma, kule pembeni kule, yeye ametoka Michigan, akiugua ugonjwa wa shida ya wanawake. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaweza kupokea uliyoomba, basi. Unaamini jambo hilo? Amina. Inua mkono wako juu, sema, "Nakukubali." Vema, unaweza kwenda zako nyumbani ukaponywe. Simjui mwanamke huyu, bali Mungu anamjua.

423 Vipi wewe hapa kwenye machela haya? Wewe ndiye tu mtu aliyelemaa, ama mtu aliye katika machela. Mimi ni mgeni kwako. Sikujui. Mungu anakujua. Lakini, nasema sasa, umefunikwa uvuli wa mauti. Una kansa. Umetoka mbali sana. Umetoka Cincinnati, hapa. Jina lako ni Bw. Hawk. Amini kwa moyo wako wote. Kama ukiketi hapo, utakufa. Mkubali Yesu Kristo nawe utaponywa. Unamwamini? Basi simama kwa miguu yako, utoke kwenye machela hayo, na ukamkubali Yesu Kristo.

424 Ni wangapi humu ndani wanaomwamini Yeye, katika dakika hii? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini kwa mioyo yenu yote? ["Amina."] Basi hebu, kila mmoja wenu, asimame sasa hivi. Simameni. Sasa katika njia yenu wenyewe, vile mnavyoomba, wewe wekelea mikono mtu aliye karibu nawe.

425 Yuko wapi Dada Brown? Amekuwa akiketi hapa, akiugua kwa huo. Hivi majuzi alinipigia simu, naye hakuweza kuinua

mkono wake. Niliona kwamba damu yake ilikuwa na kasoro fulani. Nilipokutana naye juzijuzi. . . Yeye ana ugonjwa wa sukari. Yuko wapi? Yeye alikuwa hapa na Bibi Dauch, muda kitambo uliopita. Vema, Dada Brown. Usiku wa leo, nataka uamini kwa moyo wako wote. Najua unajua una kasoro gani, bali nataka uamini. Umetoka hospitalini, upate kuja hapa, unaona, upate kuombewa. Mimi ninakuombea sasa. Amini. Utapata afya.

426 Margie, mwamini Mungu. Utaondoka sasa hivi. Utaisha. Yeye anaweza kuponya ugonjwa wa sukari, anaweza kukuponya wewe huo ugonjwa wa tumbo.

427 Sasa kila mmoja wenu amwekelee mwingine mikono, na ushikilie tu mkono wako pale kwa dakika moja tu. Wekeleaneni mikono mmoja juu ya mwingine, shikilieni. . . Mnaona, inaelekea saa tano, na wengi wa watu hawa hawana budi kuendesha hata Tennessee na mahali mbalimbali.

428 Kweli, Bwana Mungu amethibitisha. Mliona nini, usiku huu? Ulimwona mwanadamu ama ulimwona Yesu, Yesu akithibitisha Neno Lake?

429 Leso hizi zilizowekwa hapa, wakati upako huu uko juu yangu, naiweka mikono yangu juu ya leso hizi, nikiomba ya kwamba Mwenyezi Mungu. . . Wao walisema, "Walichukua kutoka katika mwili wa Paulo leso, ama vitambaa."

430 Hawa hapa waliokuwa wamekufa, nao wamefufuliwa. Wapo hapa waliokuwa katika ajali za barabarani, wakapondwapondwa, nao wameponywa. Kuna. . .

431 Ninamwona Bibi Wilson amesimama hapa, ambaye, si muda mrefu uliopita, alikuwa akitokwa na damu nusura afe, akiwa na TB, miaka kadha iliyopita. Huyu hapa usiku wa leo, madaktari hawakumpa ila masaa kadha tu ya kuishi. Huyu hapa amesimama hapa usiku huu.

432 Kila mahali, kupitia hapa, viwete, vipofu, walemavu, walio kwenye viti vya kusukumia wagonjwa na kila kitu, hao hapo wamesimama kama kumbukumbu zilizo hai. Kwa nini? Yesu Kristo yu hai, Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

433 Mtu huyo aliyetoa ushuhuda sasa hivi, muda kitambo uliopita, juu yake, kule chini, ambaye alikuwa na ugonjwa wa kifafa, aliyekuwa nao miaka hiyo yote, na kila kitu, na wakati mmoja mkutanoni. Na huyo amekuwa huku, karibu miaka ishirini iliyopita; hajashikwa na kifafa tangu wakati huo. Huyo ni mmoja wa elfu kumi.

434 Yeye ni mponya. Amina. Yeye huponya. Sasa, msisisimke. Kwa imani kama ya mtoto, tu, tazameni huko Kalvari. Fungeni macho yenu mkasahau ya kwamba mko kwenye Maskani. Fungeni macho yenu mkasahau ya kwamba kuna mtu ye yote

karibu nanyi, makamtazame Yesu mpate kuona. Mwangalieni Yesu mpate kuishi.

Imeandikwa katika Neno, haleluya!
Ni kwamba tu "tutazame tupate kuishi."

Loo, "tazama upate kuishi," ndugu yangu, ishi,
Mtazame Yesu hivi sasa upate kuishi;
Imeandikwa katika Neno, haleluya!
Ni kwamba tu "utazame upate kuishi."

435 Funga macho yako usimwone mwanadamu. Funga macho yako usiyaone mambo yanayokuzunguka. Nawe tazama kupitia imani yako, aliko Yesu Kristo, kisha ujue, ya kwamba, "Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

436 Bwana Yesu, wakati watu hawa wanaomba, na, wao wameweka mikono yao mmoja juu ya mwingine. Nasi tuna-. . . tambua ya kwamba tunasimama katika Uwepo wa Yesu Kristo aliye hai na aliyefufuka, katika umbo la Roho Mtakatifu, akitufunulia sisi siri za mioyo yetu, akiyafunua mahitaji yetu, na akituahidi ya kwamba Yeye angetupa sisi mahitaji yetu iwapo tu tutaamini.

437 Wanaume kwa wamawake wameweka mikono yao mmoja juu ya mwingine. Wao wanaomba, kwa maana sisi ni wenyeji pamoja nao wa Ufalme wa Mungu. Sisi ni ndugu na dada wenzi wao katika Yesu Kristo.

438 Na, ewe Shetani, tunakujia kwa sai la Jina la Bwana Yesu. Yeye ni Upanga. Yeye Ndiye anayekatilia maradhi mbali. Yeye Ndiye anayekatilia mbali shaka. Yeye ndiye Mshindi. Sasa tunakusai, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba uwatoke watu hawa, Shetani!

439 Neno la Mungu linadhihirishwa. Linatahirisha, linaondolea mbali shaka, linaondolea mbali maradhi, na linaleta ukombozi mkamilifu. Tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atashuka juu ya watu hawa, na kuwapa nguvu za imani kuamini ya kwamba Uwepo wa Kristo mwenye nguvu zote upo hapa sasa. Tujalie, Bwana.

440 Nahukumu kila ugonjwa. Nahukumu magonjwa yote. Nahukumu kila kutokuamini. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba ya kwamba Roho Mtakatifu aheshimu niliyosema, naye apate kupitia kote katika jengo hili na kumkomboa kila mtu katika Uwepo wa Kimbinguni.

441 Inueni mikono yenu sasa na mumsifu. Nawatangaza ninyi kwamba mu wazima na kwamba mmeponywa, katika Jina la Yesu Kristo!

Tazama Aliko Yesu SWA63-1229E
(Look Away To Jesus)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 29 Desemba, 1963 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org